

KUNG'ANG'ANIA



Salamu kwa kusanyiko hili zuri hapa usiku wa leo, Dada Webster na Ndugu Green, na kusanyiko lote, washiriki wa kusanyiko hili. Daima ni majaliwa kwangu kuja kwenye nyumba ya Bwana, na halafu, usiku wa leo, kurudi tena katika moja ya makanisa Yake ya Foursquare.

² Ninakumbuka, miaka kadhaa iliyopita, wakati nilipokuja Los Angeles kwa mara ya kwanza. Nilikuwa nimesikia juu ya Dada McPherson, lakini alikuwa amepanda vipandio vya dhahabu kabla sijawa njiani. Ndipo nilipoenda Los Angeles kwa mara ya kwanza, nilipanda nikaenda Forest Lawn. Nilisikia alizikwa kule juu, ndipo nikapanda na kusimama karibu na kaburi lake, nami nikainamisha kichwa changu na kumshukuru Mungu kwa maisha mazuri. Tangu wakati huo, nimeona ubao wa Foursquare karibu katika kila taifa ambamo nimefanya umishenari. Nimekuwa na majaliwa ya kuwa humu hekaluni, nikingojea kwenye chumba chake cha kungojea. Kabla hajaenda mimbarani, alikuwa na chumba kule. Nami nimeketi mle, siku nyingi usiku, wakati nikihubiri hekaluni, na kuwazia juu ya saa ambazo huenda alikuwa ametafakari kabla hajaingia mimbarani, ule utakatifu wa kulifungua Neno la Mungu. Kuwa hapa, usiku wa leo, pamoja na baadhi ya wafuasi wanaojaribu kuudumisha ujumbe huo ukiwa hai: Mungu awe pamoja nanyi, mbarikiwe.

³ Halafu kurudi pamoja na Ndugu Green, rafiki mpendwa, wa thamani, Ndugu na Dada Green. Basi nilipokuwa huko nje, muda mfupi uliopita, na kukutana naye, ni—nilimwambia jinsi nilivyofurahia ujumbe huo katika wimbo, hivi majuzi, huko juu kwa wafanyabiashara, kuhusu, *Jina La Yesu*, ama kitu fulani, alivyouta. Hawajaurekodi bado. Nilimwambia, “Acha niwe mteja wa kwanza,” ulikuwa ni ninii sana, wimbo mzuri sana.

⁴ Nami nilifikiri huenda wakaniambia usiku wa leo nitakaposhuka huku, na—na mke wangu na watoto wako kule nyuma kuusikiliza. Nami nina hakika waliufurahia pia. Nayo sauti yake si... Inajulikana sana huko kwetu. Nina santuri zake nyingi. Ninapojisikia vibaya sana, mimi huingia, nina moja ya hizo santuri, nami ninaweka lundo zima la sahani zake za santuri, na kuketi tu kitako na kuzisikiliza. Ninataka kumwambia mke wangu kule nyuma, ndio kwanza nimepata zingine zake. Hakika nazifurahia. Hizo ni... Ni mahali pa raha, kuzisikiliza tu hizo nyimbo za Injili, kujua kwamba zinaimbwa sio kwa sauti zilizofunzwa kimitambo, bali kutoka kwenye moyo wa Mkristo halisi.

⁵ Yeye aliniambia alikuwa bado ana zingine huko nje usiku wa leo. Ninataka mke wangu, hao, aziangalie, aone kama kuna zozote alizo nazo huko, ambazo hatuna, na ahakikishe kuzichukua. Nafikiri wanazo kwenye ukumbi. Nao . . .

⁶ Mwajua, jambo muhimu, ni kile ninachowazia juu ya uimbaji, ninazipenda hizi. Ninapenda sauti zilizofunzwa, bali sipendi sauti iliyofunzwa kupita kiasi. Ndipo unaona tu ungeweza kuishikilia pumzi yako muda gani, hata unakuwa samawati usoni, wala hata hivyo husemi chochote. Bali napenda uimbaji mzuri wa kale wa kipentekoste, ambapo unaachilia tu na kuimba. Na—napenda hilo. Naye Ndugu Green ana hiyo, yeye na Dada Green. Na kwa hiyo tunajua kwamba hizo zinaungwa mkono na kwaya hizi, na kadhalika. Na ni vizuri sana kujua hilo, vitu hivi, tunaweza kuvipata.

⁷ Sasa, mimi na Ndugu—Ndugu Green tulikutana kwa mara ya kwanza, ninaamini, ninavyoweza kukumbuka, ninaamini ilikuwa ni katika Jiji la Kansas, wakati tulipokuwa na mikutano huko nje. Jinsi nilivyokuwa nikitoka nje. . . Wao walisema, “Vema, bado sio wakati wa kuja.” Lakini ningengojea huko nje kwenye gari langu, nami nilitaka kuwa na hakika nausia uimbaji huo, wakati yeye—yeye na dada walipokuwa wakiimba.

⁸ Kwa hiyo nikamwambia huko nje, nikasema, “Ninatumaini, ya kwamba, baadhi ya siku hizi nitakapouvuka ule mto . . .”

⁹ Napenda kuimba, vizuri sana! Na mimi—mimi siwezi kabisa kuimba. Hivyo tu. Daima nimetaka kuimba, wala si—siwezi kabisa kuimba. Nami nilikuwa najaribu kuimba wimbo fulani kanisani, “Mkutano wa mtindo wa kale katika mahali pa mtindo wa kale.” Ningeuvuruga kabisa. Ningeushika tu mkono wa mke wangu nilipofika nyumbani, niseme, “Kipenzi, kamwe sitajaribu tena, basi anisaidie.” Ninapata tu . . . kila mtu mwingine amevurugika kabisa.

¹⁰ Lakini moja ya siku hizi nitaimba. Nami sikuzote nimewazia, labda huko kando ya kilima, ambapo ule—ule mto wa Uzima hushuka kupitia karibu na kile Kiti cha Enzi; wakati ile kwaya kuu ya wote waliokombolewa, sauti hizo kuu zitakapokuwa kule kando ya kilima, zikiimba. Natumaini kuna kivuli kidogo cha mti ng’ambo ya pili. Ukitaka kuniona, njoo tu karibu na pale. Nitakuwa nimeketi pale, nikiwasikiliza.

¹¹ Lakini basi utakapofika kwenye ikulu yako, asubuhi moja, na kutembea barazani mwa ikulu yako; basi huko chini mahali fulani, huko chini mwituni, kuna banda dogo lililojengwa mahali fulani. Nitainii . . . Ukitoka barazani mwako na kumsikia mtu fulani akiimba, “Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu.” Useme, “Loo, Ndugu Branham alifaulu, maana huyo hapo. Ha—hatimaye aliwasili.” Kwa hiyo nitaweza kuimba basi. Mpaka wakati huo inanibidi tu kumpigia Bwana kelele za shangwe.

¹² Hivi si tuna furaha? Hatuna kitu cha kuhangaikia, hata kidogo. Tumetia nanga katika Kristo, tukiketi katika mahali pa Mbinguni, tumetwaliwa katika neema ya Unyakuo sasa hivi, tukiketi katika Uwepo Wake mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu. Mauti yenyewe hayawezi kutugusa. Tumetiwa nanga kabisa, hakuna kinachoweza kutusumbua, kwa urahisi tuko salama tukikungojea Kuja Kwake. Nasi tunashukuru kwa hili.

¹³ Sasa, nina yapata maili mia moja na hamsini ya kuendesha gari usiku wa leo, na baada ya ibada. Na kukiwako na umati mzuri kama huu, basi inanichukua muda mrefu kuanza, na halafu maradufu yake kumalizia. Na kwa hiyo nitajaribu kuingia moja kwa moja kusema yale nimepanga kusema, upesi iwezekanavyo. Ninataka kumshukuru mchungaji, wenzake na wote, kwa ajili ya fursa hii ya kuja hapa, kutoa ushuhuda wangu wa neema Yake usiku wa leo, katika kusanyiko hili zuri.

¹⁴ Nilipanda, wakati fulani uliopita, juu ya Mlima Kusini, nikaangalia chini kwenye bonde. Nikawazia juu ya yapata miaka thelathini na mitano iliyopita wakati nilipoingia kwenye bonde hili kwa mara ya kwanza. Jinsi mji huu umepanuka, umeenea kabisa kote kwenye Bonde la Maricopa hapa. Mbali kadiri unavyoweza kuona, ni mji. Nilikuwa nimeketi pale pamoja na mke wangu, nami nikasema, “Unajua, mpenzi, labda yapata miaka mia tatu iliyopita, hapakuwapo na chochote kilichotimua mbio hapa ila mbwa mwitu na nguruwe mwitu, na kadhalika, huko kote nchini. Kisha mwanadamu akaingia akaanza kujenga. Ndipo ustaarabu ukaanza kuenea. Halafu dhambi na vurugu zikaingia.”

¹⁵ Nikawaza, “Hapa si pangekuwa ni mahali pazuri sana?” Sikuzote nimefikiria siku moja ningetaka kuishi Phoenix. Na halafu mimi... nikiangalia chini bondeni, karibu, moyoni mwangu, ningejisikia kulia, kwamba pangekuwa ni mahali pa kupendeza jinsi gani kama pangekuwa hapa bila dhambi.

¹⁶ Jinsi ambavyo wamelichukua tu jangwa na kuligeuza kuwa m—mtaa wa kuishi! Leo hii tulikuwa tunaendesha huku juu ya kichwa cha Mgongongamia, makazi ya kupendeza huko juu, ni karibu kana kwamba unaingia paradiso. Na halafu pangekuwa ni pa kupendeza, bali dhambi iko hapa kila mahali: vilabu vya wiski, utovu wa uadilifu, kila kitu tu kilicho kibaya, kila namna ya vifaa, na mitego ya adui, kuzinasa nafsi za binadamu.

Mke wangu akasema, “Basi kwa nini wewe uko hapa, Billy?”

¹⁷ Nikasema, “Mpenzi, ni kweusi. Lakini, wajua, kunao, kote katika giza hilo huko chini, kuna sehemu ndogo za Nuru. Hao ni wateule wa Mungu. Nami nipo hapa kuweka bega langu pamoja na yao, kuweka moyo wangu pamoja na yao, sauti yangu pamoja na zao, na kulikemea hilo giza.”

¹⁸ Hiyo ndiyo sababu niko hapa Phoenix tena. Mungu wa Mbinguni na atusaidie. Ndipo baada ya usiku kumalizika, na

mkutano wetu mdogo unaopitia mjini, kutoka kanisa hadi kanisa, miongoni mwa madhehebu yote ya full Gospel. Nao waliishia na mkutano wa wafanyabiashara huko Ramada. Natumaini kwamba tutaacha alama hapa, ambayo itamaanisha kwamba katika Nuru ndogo ambayo imetawanywa, kwamba nafsi nyingi zitampokea Kristo, watu wengi wagonjwa wa imani wataponywa. Tayari tumeanza kuona, kuonyesha matokeo.

¹⁹ Nami ninatumaini, usiku wa leo, kama kuna yeyote angekuja hapa usiku wa leo, chini ya uangalizi huu wa—wa kimbilio la mahali hapa, kwamba jambo fulani litasemwa katika wimbo, ushuhuda, ama kusomwa kwa Neno, ama kitu fulani, kitakachokufanya utoke nje ya mlango mtu tofauti na ulivyoingia. Litusaidie sote kufanya hivyo.

²⁰ Na sasa kabla hatujalikaribia Neno, hebu na tumwendee Mwandishi wake kwa njia ya maombi. Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja. Huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa mbele za Mungu, kungeweza kuwa na haja miongoni mwa watu usiku wa leo, kwamba una kitu fulani maalum ambacho ungetaka kumwomba Bwana akusaidie? Inua tu mkono wako. Na huko chini kabisa moyoni mwako, useme, “Bwana, Wewe unajua ni kitu gani.” Asanteni. Mungu awabariki.

²¹ Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja sasa katika Jina hilo litoshelezalo kwa yote, Bwana Yesu, tukijua hivi ya kwamba Yeye aliahidi, “Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, mtapewa.” Tunakuja, kwanza, kukiri ya kwamba tumekosea. Tumefanya makosa. Na hakuna yeyote kati yetu aliye mwema, si hata mmoja. Nasi tunakuja kuziungama dhambi zetu, katika Jina la Bwana Yesu. Tunaomba msamaha.

²² Na Wewe uliona mikono ya hao watu, iliyoinuliwa usiku wa leo, na Wewe unajua kilichokuwa chini ya mkono huo, walichohitaji. Nami ninatoa maombi yangu pamoja na yao, nikiyaweka juu ya madhabahu Yako, na nikiomba rehema, kwamba Wewe, Bwana, utatupa rehema, na utajibu kila ombi.

²³ Tunataka kukushukuru Wewe kwa ajili ya kanisa hili, kwa ajili ya wachungaji wake, na kwa ajili ya washirika wote, na mashemasi wote na wadhamini, na wote wajao. Wabariki, Bwana. Nasi tunajua ya kwamba mikutano yetu na kukusanyika pamoja kwa jumla kungekuwa ni bure, kama Wewe hukukutana nasi.

²⁴ Kwa hiyo tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba tunalo hakikisho sasa ya kwamba Wewe upo pamoja nasi. Endelea, Ee Bwana, kuwa pamoja nasi usiku kucha. Tusaidie. Ikiwa, kwa bahati, kuna wale waliokuja kutoka mtaani, ama mipakani na njia za kando za ulimwengu, ambao wamekuwa, maishani mwao, hawakujali Wewe, jalia huu uwe ndio usiku ule ambao

watamwambia Mungu ile “ndiyo” itoshelezayo kwa yote, na kujisalimisha, wajitolee kwa Yesu Kristo.

²⁵ Kukiwako na wagonjwa miongoni mwetu, Bwana, Wewe ndiwe Tabibu Yule ambaye hajawahi kushindwa kesi.

²⁶ Tunawazia siku tunayoishi, wakati maradhi na giza kuu linaifunika nchi. Lakini tunawazia tena kwamba wakati Wewe ulipokuwa ukiwaongoza watu Wako, Musa aliwatoa kutoka—kutoka Misri, akiwapeleka kwenye nchi ya ahadi, na kote katika safari kwa miaka arobaini. Ndipo walipoingia katika nchi ya ahadi hapakuwapo na mnyonge miongoni mwao.

²⁷ Ni matabibu wangapi usiku wa leo wangetaka kuyaangalia maagizo aliyokuwa nayo Musa, yaliyowadumisha watu hao na afya kwa kipindi kirefu cha miaka arobaini. Na, hata hivyo, Wewe hujayaficha. Umetujulisha yote, nayo yameandikwa hapa kwenye hizi kurasa, kwa urahisi sana. “Mimi ndimi Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote.” Jalia tutambue hilo usiku wa leo, Bwana, walio wagonjwa na wahitaji, na tujue kwamba hakuna ugonjwa ila ule Wewe uliye tiba yake, tiba maradufu.

²⁸ Bariiki kusomwa kwa Neno Lako. Na jalia mioyo yetu sasa iingie kwenye uzito wa mkutano huu. Kuanzia mioyo yetu kujazwa na furaha juu ya ule uimbaji wa Injili, na shuhuda, na kadhalika, tunashukuru tu sana. Sasa jalia tulisikie Neno Lako. Na unene nasi, Baba, na ubariki muhtasari huu kidogo ambao umeandaliwa kwa ajili ya jioni, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

²⁹ Kunao watu wengi ambao, wakija kwenye ibada, wanapenda kuandika yale mhudumu asemayo, ama kusoma kutoka kwenye Maandiko. Basi mkifanya hivyo, ninawatakeni mfungue pamoja nami usiku wa leo kwa ajili ya usomaji mdogo tu unaopatikana katika Kitabu cha Injili ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa 15, kifungu cha 21 hadi cha 28. Ningelisoma hili.

Yesu akaondoka huko, akaenda kando pande za Tiro ya Sidoni—Sidoni.

Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, . . . Unirehemu, Ee Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo.

Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu.

Akajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.

Naye akaja akamsujudia, akisema, Bwana, unisaidie.

Akajibu, akasema, Si vema kwangu mimi kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.

...akasema, Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula...makombo yaangukayo mezani pa bwana zao.

Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa; na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.

³⁰ Kama ningeliita hili somo, ningetaka kuzungumza kwa muda mfupi tu, ama kwa dakika chache, hasa, juu ya somo la: *Kung'ang'ania*.

³¹ Niliwazia, kwa kuwa Bibi McPherson na hili kanisa sikuzote wameutetea kishujaa sana uponyaji wa Kiungu, na hatuwezi kuihubiri Injili yote pasipo kuhubiri uponyaji wa Kiungu, kwa sababu ni sehemu ya Injili.

³² Ninakumbuka, kama mvulana mdogo, nikisoma makala katika moja ya magazeti, *Life* ama *Look*, ama baadhi ya magazeti hayo. Nilikuwa tu mtoto mdogo. Kuhusu wao kumdhihaki Bibi McPherson, juu ya kuhuburi uponyaji wa Kiungu, nao walisema kwamba alikuwa na u—ujanja aliofanya. Kasema, “Wanawake waliokuwa na tezi; yeye aliweka sindano chini ya kidole chake, nao wanawake wakaweka puto chini ya vazi lake. Ndipo Bibi McPherson angeweka mikono juu ya huyo mwanamke, angeichoma hiyo—hiyo puto kwa sindano, nayo puto ingetoka pumzi.

³³ Nilikuwa mwenye dhambi, bali nilikuwa na akili bora kuliko hiyo, kuwazia jambo kama hilo. Kama hiyo pini ingaliichoma hiyo puto, ingalipasuka. Kwa hiyo nikasema, “Hapana shaka ila kwamba huyo mwanamke anapata mateso.” Halafu basi, tangu nimekuwa mfanya kazi katika shamba la mzabibu, ninatambua yale yaliyombidi kustahimili. Ukiitetea kweli, sikuzote unachukiwa na adui.

³⁴ Neno *mng'ang'anizi* linamaanisha kuwa, nafikiri, kulingana na Webster, “mvumilivu.” Kuwa *mng'ang'anizi*, “kuvumilia katika kutimiza lengo.” Na kila mtu duniani, ama aliyewahi kuwako duniani, aliyepata kufanikisha chochote, ilimbidi... aliyepata kuwa chochote, ilibidi awe *mng'ang'anizi*. Inakubidi kuwa na hakika, kwanza, kile umetilia nanga imani yako.

³⁵ Sasa, imani sio kitu tu kinachoelea huku na huku kwa urahisi, na namna fulani ya...tungeliita, kwa msamiati wa mtaani, udanganyifu. Imani inaweza tu kupata mahali pa—pake sahihi wakati imewekwa juu ya kitu kilicho imara.

³⁶ Kama ningalikwambia uondoke uende ukaweke mkono wako juu ya mti ule upate kuponywa, ungeshuku hilo. Kwa hiyo, kwa nini? Hatuna msingi kwa chochote. Ungekuwa tu na neno langu. Na kama nilikwambia ya kwamba kuoga katika maji fulani hapa nje bo—bondeni kungekufanya uponywe, ingetegemea imani uliyo nayo kwangu.

37 “Na imani chanzo chake ni kusikia.” Kusikia nini? “Neno la Mungu.”

38 Kwa hiyo, kama *Hili* ni Neno la Mungu, nalo Ndilo, yale linayofundisha tunaweza kuyategemea. Mungu hawezi kubadilika. Mungu hana budi milele kudumu Mungu. Neno Lake halina budi kuwa kweli katika wakati huu kadiri lilivyowahi kuwa katika wakati wowote.

39 Sasa, sisi tuna kikomo. Tunaweza kusema jambo fulani mwaka huu, na labda hata kesho itulazimu kulibadilisha. Kwa sababu, hatuna uhakika sana, kwa sababu sisi tuna kikomo. Tunadhania tu. Na *kudhania* linamaanisha “kudiriki pasipo mamlaka.”

40 Lakini Mungu anaposema jambo lolote, ni kamilifu. Haimbidi kulibadilisha. “Ibrahimu hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; bali alitiwa nguvu, akimsifu Mungu, kwa sababu alijua kwamba Yeye aliweza kutenda, ama kutimiza, ama kufanya yale Yeye aliyokuwa ameahidi.” Halafu, kama Mungu akiwahi kuitwa jukwaani atoe uamuzi, basi uamuzi ambao Mungu anatoa, kwanza, hauna budi kudumu vivyo hivyo milele. Kamwe hauwezi kubadilika. Hauwezi kubadilishwa, kwa sababu Yeye hana kikomo. Na chochote kisicho na kikomo kamwe hakikuwa na mwanzo wala mwisho. Kwa hiyo Yeye hawezi akaughairi mwaka ujao, na kusema, “Nilikuwa nimekosea.”

41 Halafu basi ikiwa huo ulikuwa ndio uamuzi Wake, basi kila mtu anayefanya uo huo, uh, anafikia uamuzi uo huo alioutoa Mungu kwa ajili ya mtu mmoja juu ya msingi wa imani yake, kuuamini, Yeye hana budi kutimiza jambo lilo hilo kila wakati mtu anapoliamini. Mungu hana budi kutenda, kila wakati, jinsi alivyotenda mara ya kwanza, la sivyo Yeye alitenda vibaya wakati wa kwanza. Basi ni nani anayeweza kumshtaki Mungu kwa kutenda vibaya? Mungu hana budi daima kudumu na uamuzi Wake.

42 “Kama unaweza kuamini!” Sasa, kufanikisha lolote, inakubidi kuweka lengo na kusema, “*Hili* ninaamini,” na kujifunganisha kwake, na kuendelea kujongea, kulikaribia, ukijua ya kwamba umeninii...liko hapo, ukijua kwamba kuna kitu fulani pale ambacho unakiendea.

43 Kama vile ilivyosemwa, yule mvulana mdogo aliyekuwa na tiara, ameshika kamba mkononi mwake. Alisema, huyo mtu alisema, “Kwani umeshika nini, mwanangu?”

Akasema, “Tiara yangu.”

Akasema, “Sioni kitu ila kamba.”

Akasema, “Lakini kuna tiara mwishoni mwake.”

Mtu huyo akaangalia juu, kasema, “Siioni hiyo tiara.”

Mvulana huyo mdogo akasema, “Wala na mimi.”

Akasema, “Vema, unajua je una tiara?”

Akasema, “Ninaweza kuihisi ikivuta kwa nguvu huko mwisho.”

⁴⁴ Vema, hivyo ndivyo imani ilivyo. “Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.” Mradi tu umeweka imani yako juu yake, kisha ukatia nanga kwake, unaiendea. Haidhuru kama huwezi kuiona, ama la, unajua iko kwa vyovyote vile. Unaivuta kwa nguvu, nayo inakuvuta. Na mtu yeyote aliyepata kufanya jambo lolote muhimu, ameweka lengo, halafu ameng’ang’ania, akavumilia, kufanikisha hilo: watu mashuhuri.

⁴⁵ George Washington, “baba wa taifa letu,” anavyoitwa, wakati alipofika kwenye Bonde la Forge, baada ya usiku kucha katika maombi, mpaka akalowa kwa theluji, kufikia juu ya nyonga zake, huku amepiga magoti kwenye theluji, kesho yake asubuhi alivuka Delaware, uliojaa barafu. Kwa nini? Alikuwa mng’ang’anizi. Alikuwa na jibu. Hakuna kitu kitakachomzuia. Ingawa ninii tatu ama nne za gobori. . . risasi za gobori zilipitia kwenye koti lake, bali hazikumdhuru. Yeye alijaribu. . . Alitaka kufanikisha jambo fulani, naye alikuwa ameliombea akafaulu, pia alikuwa mng’ang’anizi. Hakuna kitu kilichomzuia.

⁴⁶ Ungeweza kuwazia Nuhu katika siku zake, jinsi Nuhu alivyoshikilia? Sasa, yeye alikuwa ni mkulima tu.

⁴⁷ Nao waliishi katika siku bora zaidi za utafiti wa kisayansi, labda, kuliko tulizo nazo siku hizi, kwa sababu katika zama hizo wao walijenga piramidi. Na endapo mmoja wenu amekuwa na majaliwa ya kuwa kwenye ile piramidi kuu ya Misri na kuiona ile Sfiniksi na kadhalika, mbona, ni tamasha la kushangaza. Jinsi walivyoweza kuyanyanyua majabali hayo huko juu hewani, karibu urefu wa jengo la mji kwenda juu, yenye uzito wa maelfu ya tani! Leo hii tusingeweza kuzijenga tena. Hatuelewi. Walikuwa na kitu fulani.

⁴⁸ Walikuwa na rangi. Walikuwa na kitu wangaliweza kuuhifadhia mwili, ambacho kingeufanya uonekane wa kawaida kabisa kwa maelfu ya miaka. Hatuna hizo sanaa, kutia rangi, na kadhalika, walizokuwa nazo; wakati mkuu wa kisayansi.

⁴⁹ Lakini siku moja, wakati Nuhu alipokuwa huko nje ko—kondeni, labda akishughulikia mimea yake, Mungu alimtokea akamwambia, “Jiandae kwa ajili ya wokovu wa nyumba yako, na ujenge safina. Nako kutanyesha.”

⁵⁰ Sasa, sote tunajua hivyo, ule ulimwengu uliotangulia gharika, hakukuwa kumenyesha. Na sasa, huo haukuendana na wataalamu wa kisayansi wa siku hizo. Ujumbe wake ulikuwa kinyume. Hapana shaka kwamba wanasayansi werevu wangaliweza kumjia na kusema, “Sasa, angalia hapa, Bw. Nuhu. Sasa tuna zana tunazoweza kurusha mwezini, nasi tunaweza kufanya utafiti huu wote wa kisayansi. Wala hamna maji huko

juu. Basi maji yoyote yatakuja kutoka kule, wakati hamna maji huko juu ya kumwagika chini? Wewe ni mpumbavu. Unafanya kazi bure. Hamna maji huko juu.”

⁵¹ Lakini Nuhu angeweza kusema, “Mungu alisema kwamba itanyesha, na hilo latosha. Mungu alisema hivyo.” Miaka mia moja na ishirini, aling’ang’ania mbele ya ulimwengu wa kisayansi wa siku zake, angali akidai ujumbe wake ulikuwa ni wa kweli kwa kuwa ulitoka kwa Mungu. Alikuwa na lengo la kutimiza. Alikuwa na ujumbe wa kushughulikia, naye alishikilia katika kufanya hivyo. Haijalishi yale ulimwengu wote uliyosema, Nuhu alisikia kutoka kwa Mungu. Hilo ndilo tu lililojalisha kwake. Alikuwa ameisikia Sauti. Alikuwa na hakika ilikuwa ni Mungu, naye alikuwa akitayarisha kitu kilichoonekana cha kijinga sana mbele ya ulimwengu. Lakini, hata hivyo, Nuhu alijua ya kwamba Mungu angelitimiza Neno Lake.

⁵² Hivi hilo halipaswi kuwa ni somo kwetu siku hizi, saa hii? Kama Yesu alivyosema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Ujumbe ambao ni wa kipumbavu, kwa ulimwengu. Hawaelewi. Lakini hata hivyo wale waliowasiliana na Roho Mtakatifu, wanajua ya kwamba Yeye atarudi tena.

⁵³ Ninaweza kuwaona watu hao wakati wakimhurumia maskini mzee Nuhu, kuhusu jinsi alivyokosa burudani nyingi, na ya ulimwengu na mambo yaliyokuwa yakiendelea. Lakini Nuhu, akiwa angali anang’ang’ania, alishikilia moja kwa moja.

⁵⁴ Siku moja Mungu akamwambia Nuhu, “Vema, umefanya sehemu yako sasa. Sasa ingia ndani ya safina, wewe na nyumba yako.” Na ninii. . . Wakaona nde—ndege wakianza kuruka ndani, na—nao wanyama wakaanza kuingia, wawili-wawili. Nuhu na familia yake wakaingia.

⁵⁵ Na sikuzote kuna waaminio wakwamia mpakani, ninavyowaita; watu watakaokuja kanisani, watafurahia ujumbe labda kutoka kwenye kwaya ama kutoka kwa waimbaji, kutoka kwa mhudumu, ama ushuhuda. Watafurahia, bali, kuingia na kuwa sehemu yake, kamwe hawataingia. Wanapenda kusikiliza, bali hawatakuwa sehemu yake. Hawataki kutambulishwa pamoja nao. Wanataka kukaa upande mmoja. Imekuwa hivyo sikuzote, na hapana shaka walikuwako siku hizo.

⁵⁶ Ndipo mlango wa safina ulipofungwa, wengi wa watu hao wakasema, “Vema, hebu tupande tukasimame pale karibu, sasa, ikitokea kwamba, kwa mfano, huyo mzee alisema kweli. Sote tulidhania kwamba huyo mzee kidogo alikuwa amerukwa na akili, bali ni—ni—nilifurahia kumsikia akihubiri, akisimama pale mlango. Na sasa tunajua kwamba kitu fulani kiliufunga mlango ule. Sasa, yeye ni mzee mzuri. Na kama ikitokea, maji

yashuke chini huko juu, mbona, mbona, atatukaribisha ndani.” Mnaona, hutaki kutumainia . . .

⁵⁷ Hutaki kuuchosha wema wa Mungu. Unataka kuhakikisha ya kwamba unaingia tu wakati ukiwa na nafasi ya kuingia.

⁵⁸ Halafu, muda si muda mwajua, siku ya kwanza, angalia jinsi Mungu anavyowachosha watu Wake, wakati mwingine, ningewazia, siku ya kwanza, Nuhu aliiambia familia yake, “Vema, sasa tutapanda juu kwenye orofa ya juu. Sasa, asubuhi, anga zitakuwa na giza. Hakujawahi kuwa na giza hapo kabla. Hatujawahi kuliona. Mvua itanyesha. Radi itamulika angani.” Ndipo kesho yake asubuhi hilo hapo jua linachomoza. Hakuna ishara. Siku nzima, Nuhu na familia yake walitazama. Vema, mambo yaliendelea jinsi tu yalivyokuwa.

⁵⁹ Ninawazia waumini wakwamia mpakani walisema, “Ai, maskini huyo mzee alikosea.” Wakashuka wakarudi katikati ya mji, wakila, wakinywa, na kujifurahisha.

⁶⁰ Ninawazia, familia yake, ni jambo la kuchosha jinsi gani hapana shaka hilo lilikuwa kwa huyo mtu. Lakini hakukata tamaa na kuanza kugonga mlangoni, na kusema, “Enyi watu, bandueni mlango ufunguke. Nilikosea.” Kwa nini? Alijua alikuwa na ukweli, naye akaushikilia.

⁶¹ “Endapo haikunyesha leo, itanyesha kesho.” Jambo ndilo hilo. Vema.

⁶² Basi siku ya pili ikaja, nasi tunaona jua lilichomoza. Lilivuka tu kama lilivyofanya kila siku. Hakuna ishara ya mvua. Angali alishikilia. Moja kwa moja kufikia siku saba, Nuhu alikuwa ameketi pale pale, kasema, “Endapo haikunyesha leo, itanyesha kesho.” Mnaona, yeye alikuwa ametia nanga. Alikuwa aking’ang’ania, mvumilivu, kwa kuwa alijua ya kwamba Mungu alisema hivyo, na ilibidi iwe hivyo.

⁶³ Sasa, hatimaye, kwenye siku ya saba, wakati alipoangalia nje ya dirisha, anga zilianza kuwa nyeusi. Upepo ulikuwa ukivuma kupitia milimani. Miti ilikuwa ikiinama. Watu walikuwa wakipiga mayowe, wasijue la kufanya. Na baada ya kitambo kidogo, matone makubwa mno ya mvua yakaanza kuanguka chini kwa mara ya kwanza, yakiipiga mitaa. Mifereji ya majitaka ikajaa. Chemchemi zote zikapasuka. Maji yakaanza kuinuka. Watu wakaingia kwenye mitumbwi yao, nayo ikazama. Pepo zilikuwa kali. Na yakapata kina kikubwa zaidi, na zaidi, na zaidi. Baada ya kitambo kidogo, yakaanza kupanda kwenye ile meli. Yeye akaangalia dirishani.

⁶⁴ Hatimaye, huku watu wakipiga mayowe, hana njia ya kunyosha mkono na kuwafikia. Yeye alikuwa huko juu kabisa kwenye orofa ya juu. Walikuwa wametenda dhambi wakamalizia siku yao ya neema. Hakuna nyingine iliyosalia kwa ajili yao. Ilikuwa imechelewa sana wakati huo. Hatimaye, ni hisia ya jinsi gani hapana shaka hiyo ilikuwa, kwa Nuhu, wakati alipoangalia

nje mtaani na kuona zile mashua zote ndogo, kama zilikuwa zimetengenezwa na Mungu ama la.

⁶⁵ Mnaona, watu wanafikiri hivyo siku hizi. “Wanaweza kutengeneza safina yao wenyewe. Wanaweza kufanya wokovu wao wenyewe.” Huwezi kufanya jambo hilo. Mungu alifanya wokovu kwa ajili yetu, nasi hatuna budi kuukubali. Safina tu iliyotengenezwa na mwanadamu haitastahimili. Chochote ambacho mwanadamu anaweza kufanikisha, ambacho ni kinyume na mapenzi na Neno la Mungu, hakitasimama.

⁶⁶ Lakini jinsi hapana shaka ilikuwa wakati Bibi Nuhu na wake za wanawe, na—na mwana—wanawe, na kadhalika, walipoyaona maji haya yakipanda juu kwenye safina, na hata hivyo safina ilikuwa ingali imekaa ardhini. Lakini baada ya kitambo kidogo waliisikia imejinasua. Ikaanza kuelea. Loo, Nuhu alijua ya kwamba yote yake, yale aliyokuwa amejaribu kufanikisha, yale aliyokuwa amefanya, ujumbe wake ulikuwa ukizaa matunda basi. Ilinasuka. Alikuwa akiondoka ardhini.

⁶⁷ Kama vile ilivyo wakati mtu atakaa, sio kuja na kupeana mikono na mchungaji, kuandika jina lake kwenye kitabu, bali wakati atakapokaa pale mpaka asikie kitu fulani kikijinasua ndani yake, naye anaanza kuelea huko ng'ambo kwa imani, akijua ya kwamba dhambi zake zimepita, naye ametia nanga nafsi yake katika Kristo, na kuna kitu kinachomwinua juu zaidi na zaidi; kung'ang'ania, kushikilia.

⁶⁸ Musa alikuwa ni mng'ang'anizi sana, baada ya kushuka kwenda Misri na kumwua mtu, na pamoja na elimu yake yote na mafunzo yake. Na hata hivyo alifanya jambo hilo vibaya, alijaribu, sababu alitumainia yale angeweza kufanikisha kwa elimu yake na kwa nafsi yake. . . Tunaambiwa ya kwamba yeye alikuwa ni mwanajeshi. Na kile alichokuwa amefunzwa kufanya, tunaona kwamba kilishindwa. Na wakati kiliposhindwa, yeye hakuvumilia hilo, alikimbia nyikani kwa miaka arobaini.

⁶⁹ Bali wakati mmoja alikutana na Mungu katika kichaka kilichowaka moto, akavua viatu vyake, akauona utukufu wa Mungu. Aliona kijiti kikavu kikigeuka kuwa nyoka, na kurudi kikawa kijiti tena. Aliona mkono wenye ukoma ukiponywa kwa nguvu za Mungu. Naye akasikia Sauti ya Mungu ikisema naye. Hakuna kitu kitakachomzuia basi.

⁷⁰ Mara nyingi nimetoa wasifu wake. Natumaini siyo njia ya kukufuru. Maskini mzee, umri wa miaka themanini, mke wake ameketi kumtagaa nyumbu, huku m—mtoto yuko kwenye nyonga yake. Kesho yake. . . Na ndevu zikining'ania chini, fimbo mkononi mwake, akienda, macho yake yameelekezwa, na—na kuelekea angani, huku ndevu nyeupe zikipeperuka.

Ndipo mtu fulani anasema, “Kwani unaenda wapi, Musa?”

⁷¹ “Ninashuka kwenda Misri, kuiteka.” Uvamizi wa mtu mmoja, kidogo lilionekana ni dhahaka. Bali njia za Mungu,

kwa nia ya kimwili, ni dhihaka. Bali ni za thamani kwa wale waliotia nanga kwake. Wanajua kile wanachozungumzia. Wanakaza mwendo. Loo, ni jambo la jinsi gani hapana shaka hilo lilikuwa! Nuhu ama . . .

⁷² Musa, hasa, akishuka kwenda Misri, taifa lililouogopesha ulimwengu, kitu kama Urusi siku hizi. Uvamizi wa mtu mmoja, mzee, umri wa miaka themanini, huku mke wake ameketi juu ya nyumbu, na fimbo iliyopinda mkononi mwake, akishuka kwenda kuiteka. Jambo hilo, ajabu kweli, kwa ulimwengu, yeye alifanya hivyo. Aliiteka.

⁷³ Mungu anapaswa tu kuwa na mtu mmoja, mtu mmoja, mahali fulani, ambaye amefunganishwa Kwake, mtu fulani anayejua mahali wanaposimama naye ni mng'ang'anizi. Mateso basi, tofauti, hayawasumbui, hata kidogo. Akishuka kwenda kuiteka, naye aliiteka.

⁷⁴ Lilionekana la dhihaka sana wakati hapo alisimama mtu mwenye urefu wa futi kumi na nne, ama zaidi. Ninaamini, vidole vyake, urefu wa inchi kumi na nne; akiwa na mkuki mkononi mwake, kama sindano ya mfumaji, labda nusu ya hapa na mlangoni huko nje; amesimama kule, akiwapa Israeli changamoto. Kulikuwako na Sauli upande ule mwingine, kichwa na mabega juu ya jeshi lake, mtu aliyefunzwa, wote wamefunzwa vizuri, na wametishiwa. Hiyo ni kweli.

⁷⁵ Naye ibilisi alitaka kushauriana nao. Hivyo ndivyo ibilisi afanyavyo anapowazia yuna nafasi nzuri kabisa. "Njoni huku. Hebu tusimwage damu. Wawili wetu tu. Nikimshinda mtu wenu, basi tutaninii. . . ninyi mtatutumikia. Kama akiniua, basi kutakuwako na mmoja wetu tu atakayekufa badala ya majeshi yetu." Ni ushauri wa jinsi gani anaoweza kutoa! Kila mtu aliomgopa nusura afe.

⁷⁶ Na lilionekana la dhihaka kumwona maskini mtoto mdogo, mwenye mabega yaliyoinama akija huku amejizungushia ngozi ndogo ya kondoo, kombeo limefungwa ubavuni mwake, akiwa na keki za zabibu kavu mkononi mwake, kuwaona ndugu zake. Ndipo ibilisi huyo akajigamba mbele za mtu wa Mungu, wakati mmoja, naye akampa changamoto. Kwa nini? Yeye alijua Mungu alikuwa ni Nani. Kasema, "Nitaninii. . . Mnataka kuniambia kwamba mtaacha majeshi ya Mungu aliye hai kumwacha huyo Mfilisiti asiyetahiriwa ayatukane majeshi ya Mungu aliye hai? Nitaenda nikapigane naye." Loo, jamani! Kwa nini? Alikuwa aking'ang'ania.

⁷⁷ Ndugu zake wakasema, "Aa, tunajua wewe ni mtundu. Rudi nyumbani na hao kondoo baba aliokwambia uwachunge. Umekuja tu hapa kuona vita." Huwezi kumshinda kwa maongezi mtu wa Mungu, wakati kitu fulani kimekwisha tukia kwake.

⁷⁸ Kwa hiyo anapanda kwenda kwa Sauli. Sauli, nadhani, alijikuna kichwa chake akaangalia chini. Akasema, "Navutiwa

na ujasiri wako, mwanangu, lakini mtu huyo ni shujaa wa vita. Mtu huyo ni shujaa wa vita, tangu utotoni mwake. Na wewe si kitu ila kijana, wala hujui lolote kuhusu kombeo wala kuhusu mkuki, wala jinsi ya kushambulia kwa upanga.”

⁷⁹ Loo, bali hebu mwone akitambulisha kitu fulani. “Mtumishi wako aliwachunga kondoo wa baba yake.” Kisha akasema, “Siku moja dubu alikuja akamchukua mmoja wa wana-kondoo wa baba yangu, ndipo nikamfuata, na kumwua. Kisha simba akaingia na kumchukua mmoja na kuondoka naye, nami nikamfuata, nikamwua. Sasa,” akasema, “Mungu yule aliyenipa ushindi dhidi ya dubu na dhidi ya simba, ni zaidi sana vipi Yeye atanipa ushindi dhidi ya Mfilisiti huyo asiyetahiriwa ambaye anayatukana majeshi ya Mungu aliye hai!”

⁸⁰ Sauli akasema, “Lakini wewe ni mtoto tu.” Akasema, “Hujavaa chochote, maskini ngozi tu ya kondoo. Ngoja, nita—nitakuvalisha silaha zangu.”

⁸¹ Kwa hiyo akamchukua na kumvalisha silaha zake. Mngeweza kuwazia? Biblia ilisema yeye alikuwa “mwekundu,” mtu mdogo, labda mtu mwenye pauni mia moja na kumi, akivaa silaha kubwa mno za mtu angalikuwa na uzito wa mia mbili hamsini, urefu wa kama futi saba na kitu. Alipondolewa chini kabisa. Ungeweza kuwazia jambo hilo?

⁸² Daudi akaangalia kote. Mabega yamezidi kwa yapata umbali huu. Basi ilionekana kama amevaa sketi, imening’inia chini namna hiyo, deraya yake ya kifua. Alikuta kwamba hiyo fulana ya kikanisa haikumwenea mtu wa Mungu. A-ha. Kasema, “Ondoa kitu hiki kwangu. Sijui chochote kukihusu. Bali acheni niende na kile ninachojua ni sahihi.” Haya basi. Akaenda kwa nguvu za Roho.

⁸³ Naamini ilikuwa ni Hudson Taylor wakati mmoja alimwambia mmishenari wa Kichina. Mvulana huyu wa Kichina alisema, “Bw. Taylor, nimehisi wito wangu katika Kristo.” Akasema, “Niende sasa nikasomee Shahada yangu ya Sanaa, halafu niisomee Ph.D. yangu, na yote ninayopaswa kuwa nayo, digrii yangu ya uzamili?”

⁸⁴ Bw. Taylor akasema, “Nenda sasa, mwanangu. Nenda sasa. Usingoje mpaka wakati huo uje. Utapoteza wakati mwingi kupita kiasi wa maisha yako.”

⁸⁵ Nafikiri hiyo ni kweli. Ninakubaliana na Bw. Taylor. Nenda sasa. Mimi sijaribu kuunga mkono ujinga wangu sasa kwa kujaribu kusema hatuhitaji elimu. Hiyo inaweza ikawa na mahali pake. Lakini elimu pasipo na wokovu haina nanga. Ni matanga tu pasipo na nanga. Nenda wakati mshumaa umewashwa. Usingoje mpaka umechomeka nusu. Nenda wakati umeuwasha. Kama hujui chochote zaidi ya vile ulivyowashwa, waambie wengine jinsi ulivyowashwa, labda watawashwa pia. Unaona? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Kwa hiyo mara

tu mshumaa unapowashwa, nenda kamwambie kila mtu jinsi mshumaa wako ulivyowashwa, na labda watawashwa kutoka kwako. Unaona? Angalieni.

Bila shaka, Daudi alikuwa mng'ang'anizi, kwa sababu yeye alijua.

⁸⁶ Samsoni alikutwa uwanjani siku moja na Wafilisti elfu moja waliomzunguka. Akaangalia kote kwenye... Yeye hakuwa ni mtu aliyefunzwa aliyejua jinsi ya kushambulia kwa upanga. Bali alipokigeuza kichwa chake alihisi agano lile, vile vishungi vikiangukia mabega yake. Hayo ndiyo tu yaliyompasa kusikia. Akashika kitu cha kwanza mkononi mwake, kilichokuwa ni mfupa wa taya la nyumbu, naye akawapiga na kuwaangusha Wafilisti elfu moja. Kwa nini? Aling'ang'ania kwa sababu alijua ya kwamba Mungu alikuwa amefanya agano naye, la hivyo vishungi saba. Mradi tu vilining'inia mahali pao, hakuna kitu kingalimsumbua.

⁸⁷ Loo, ndugu, dada, jinsi Kanisa la Mungu aliye hai linavyopaswa kusimama usiku wa leo, liking'ang'ania. Mradi tu tunaweza kulihisi lile agano la Roho Mtakatifu, Damu ya Yesu Kristo ikitusafisha na dhambi yote, haitupasi kuacha kitu chochote kisimame mbele zetu. Kung'ang'ania, bila shaka.

⁸⁸ Yohana, yule nabii mkuu aliyenenwa habari zake, kuinuka; alipokuwa nyikani, yeye aliambiwa na Mungu. Walikuwa wakimtarajia Masihi, hakika; miaka mia nne kabla hawajawa na nabii. Lakini, Mungu alimwambia, huko nyikani, Yeye alisema, "Sasa, wao watajaribu kukwambia, 'Dk. *Fulani-wa-fulani* ndiye jamaa anayepaswa kuwa Masihi, kama unapaswa kumtangaza. Mbona, yeye ndiye mtu mzuri kuliko wote kwenye kusanyiko letu.' Nao watasema, 'Vema, m—mjukuu wa kuhani mkuu hapa juu, ndi—ndiye jamaa anayepaswa kuichukua,' na kadhalika. Lakini, angalia, Yohana, hii ni kazi kwelikweli. Huna budi kuwa na hakika, kwa hiyo nitakupa ishara. Yeye Ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, huyo Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na moto."

⁸⁹ Yohana alisimama pale, akaangalia juu ya makusanyiko walipokuwa wakija. Naye... Kila mtu akija *hivi, vile*, na *vinginevyo*. Bali yeye asingeweza kumwona. Siku moja, wakati amesimama, akijadiliana na kuhani, akisema, "Unataka kuniambia wakati utakuja ambapo dhabihu ya kila siku itaondolewa?"

Yeye akasema, "Atakuja Mtu."

⁹⁰ Naye akaangalia. Huyu hapo. Kasema, "Tazama, huyo hapo Mwana-kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu."

⁹¹ Yeye alijua hilo kwa sababu Mungu alikuwa amemwambia, "Yule utakayemwona Roho akishuka juu Yake." Yeye alijua jambo hilo. Yeye aling'ang'ania.

⁹² Turejee kwa maskini mwanamke huyu. Tunayo mambo mengi tungeweza kusema kuhusu watu mbalimbali waliokuwa wavumilivu, waking'ang'ania, wakiendelea kushikilia, kufanikisha.

⁹³ Ninao msemu mdogo, ninaosema mara nyingi. Huenda ikawa ni vizuri muuchukue. "Mshindi hatoroki, naye mwenye kutoroka hashindi." Uwazie tu. "Mshindi hatoroki, naye atorokaye hawezi kushinda." Huna budi kushikilia. Na kabla hata hujaanza, kuwa na hakika kabisa uko sahihi. Kisha ung'an'anie, usiache chochote kikusukume. Endelea. Nimekuwa na uzoefu mwingi sana wa jambo hilo, nanyi mnajua. Ninajua jambo hili moja, unapokuwa na hakika kabisa kwamba uko katika mapenzi ya Mungu, wakati unapokuwa na hakika kabisa umelenga Kalvari, hakuna kitu kitakachokutikisa. Uko pale.

⁹⁴ Maskini mwanamke huyu, alikuwa ni Myunani, na Msirofoinike, naye alikuwa amesikia sifa za Yesu. Sasa, imani huja namna gani? Kwa kusikia, kulisikia Neno. Yeye alikuwa amesikia habari Zake. Nanyi mwajua, huenda alikuwa na mambo mengi sana ya kumzuia, kwa yeye kuwa Myunani. "Imani chanzo chake ni kusikia." Tunajua hilo. Naye alikuwa na mambo me—mengi sana ya kumzuia, bali imani hupata kiini hamna yeyote mwingine anayejua kitu juu yake.

⁹⁵ Imani hupata chanzo hiki ambacho hakuna mtu anayeweza kukieleza. Ni kitu ambacho unajua. Wengine hawawezi kukiona, bali imani inakiona. Imani hukiona hicho, ambapo jicho la kawaida halikioni. Bali jicho la ndani hukiona kitu hicho.

Sasa, yeye alikuwa na haja ya Yesu. Ali- . . .

⁹⁶ Jambo la kwanza likupasalo kufanya, kama utampata Kristo, inakupasa kujua kwamba unamhitaji. Unapowazia kwamba humhitaji, basi kamwe hutampata, maana hutamtafuta kwa bidii.

⁹⁷ Hivi uliona Maandiko mahali yanaposema, "Tafuteni nanyi mtapata, bisheni nanyi mtafunguliwa"? Kwa kweli, hiyo si kubisha tu, kama [Ndugu Branham anagonga mimbarani mara moja—Mh.], nao utafunguliwa. Yeye hiyo siyo tu kusema, "Vema, nilitoka nje, Bwana. Mimi hapa. Unanitaka?" La, hivyo sivyo. "Yeye atafutaye, yeye abishaye," kuendelea. [Ndugu Branham anagonga mimbarani mara kadhaa.] Halina budi kulingana na Maandiko hayo mengine.

⁹⁸ Kama vile yule hakimku dhalimu na yule mjane. Aliendelea kuubisha mlango wake. Aling'ang'ania. Kama alimfukuza leo, kesho alikuwa mikononi mwake tena.

⁹⁹ Hivyo ndivyo unavyotaka kumpata Mungu. Kuwa mikononi Mwake, kila asubuhi, kila usiku, kila siku, wakati wote, sikuzote. Endelea tu kutafuta, endelea kuomba, endelea kubisha. Usibishe tu kidogo, kisha uchoke na kuondoka. Endelea tu kusimama hapo, "Bwana, nipo hapa, wala sitaondoka. Niko mikononi

mwako sasa. Mimi nitakaa papa hapa. Unachoka kusikiliza? Nina wakati mzuri sana nikibisha, maana ninajua Wewe unakuja.” Amina. Hapo ndipo jambo fulani hutendeka. Hana budi kukuondoa mkononi Mwake, unaona, kwa hiyo Yeye anatoka kuja kukujibu. Sasa, imani hupata hili.

¹⁰⁰ Neno Lake ni Upanga. Biblia inasema, katika Waebrania 4:12, kwamba, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili.”

¹⁰¹ Sasa, kuna kitu kimoja tu kinachoweza kuushika Upanga huu. Hicho ni mkono wa imani. Mkono wa imani ndio kitu cha pekee kinachoweza kuutumia upanga huu wa imani, upanga wa Neno. Sasa, huenda ukawa na mkono dhaifu, wa kutosha tu kuutwaa kwa ajili ya kuhesabiwa haki, wewe ni dhaifu sana. Labda hilo ndilo tu unaloweza kukata. Lakini upanga huu wa Neno utakata na kuweka huru kila ahadi ambayo Mungu alitoa ndani Yake, iwapo wana mkono mzuri wenye nguvu wa imani ukiushikilia pale. “Ninamwamini Mungu kwa ajili ya uponyaji wangu. Ninamwamini Mungu kwa ajili ya ubatizo wangu.” Mungu alitoa ahadi, nayo imani ikiushika Upanga huu, itaukata kutoka kwenye Mwamba huko ng’ambo. Kila ahadi ya Mungu inaweza kukatwa iwe huru, kwa Neno la Mungu, kwa kuwa ni Upanga.

Alikuwa na vizuizi vingi, lakini imani yake haikuwa na chochote.

¹⁰² Huenda ukawa na pingamizi nyingi. Kila mtu anayeondoka kwenda kukutana na Kristo utapata unazo pingamizi nyingi sana, bali imani yako haina yoyote. Imani haina pingamizi. Imani ina nywele kifufuani mwake, misuli mikubwa mno.

Hoja huinuka na kusema, “Unajua, ni la maana.”

¹⁰³ Imani huvuta misuli yake nyuma na kutokeza kifua chake kikubwa, na kusema, “Nyamaza. Kaa chini.” Nayo hoja inaruka huko pembeni na kuchukua stuli yake. Kweli. Imani ina misuli, na yeye—yeye anamaanisha analosema.

¹⁰⁴ Hiyo ndiyo tunayohitaji usiku wa leo. Hiyo ndiyo kanisa la Foursquare linayohitaji. Hiyo ndiyo kundi la Kipentekoste linayohitaji. Hiyo ndiyo ulimwengu mzima unayohitaji. Hiyo ndiyo ninayohitaji. Hiyo ndiyo unayohitaji. Nasi tunapaswa kujionea aibu kukubali hilo, bali tunahitaji imani itakayolishika Neno la Mungu na kusema Hilo ni kweli. Kukutana na ibilisi na kusema, “BWANA ASEMA HIVI.”

¹⁰⁵ Nilikuwa nikisoma hivi majuzi ambapo mtu mmoja alisema ibilisi alisimama mbele zake. Naye akasema, “Yeye alikuwa tu ni maskini ibilisi mdogo wa kale, naye akasema, ‘Buu.’”

¹⁰⁶ Kasema, “Niliruka nyuma.” Kisha kasema, “Akasema, ‘Buu.’ Nikaruka nyuma. Kila aliposema kwa sauti kuu, ‘Buu,’ nami nikaruka nyuma, yeye angekuwa mkubwa zaidi nami ninakuwa

mdogo zaidi.” Naye akasema, “Aliendelea kusema, ‘Buu.’” Kasema, “Ningekuwa mdogo zaidi kila niliporuka nyuma, naye angekuwa mkubwa zaidi.”

¹⁰⁷ Kasema, “Nilijua ilinibidi kupigana naye, baada ya kitambo kidogo.” Kasema, “Nikaangalia huku na huku, nikawaza, ‘Kitu gani?’ Nililipata Neno la Mungu.” Kasema, “Nikalizungusha mkononi mwangu. Ndipo ibilisi akasema, ‘Buu.’ Nami nikasema, ‘Buu,’ pia.” Basi kasema, “Niliposema, ‘Buu,’ pia, kila niliposema, ‘Buu,’ akawa mdogo zaidi nami nikawa mkubwa zaidi.” Jambo ndilo hilo. Huna budi kupigana naye, siku moja.

¹⁰⁸ Unajua, watu hawaamini kuna ibilisi. Ninakutana na yeye, wakati wote, a-ha, ninakabiliana naye kila siku. Mwaminio mwingine yeyote hukabiliana naye. Naam, huna budi kupigana naye, siku moja, kwa hiyo afadhali uanze sasa hivi. Kuna kitu kimoja tu anachoogopa, ni hiyo Damu na hilo Neno. Imani huishikilia. Ina nguvu, inasonga mbele.

¹⁰⁹ Sasa, tunaona, maskini mwanamke huyu Myunani, kama nilivyosema, yeye alikuwa na pingamizi nyingi, bali imani yake haikuwa na yoyote. Imani haina pingamizi yoyote. Huenda walimwambia, “Hivi unajua wewe ni Myunani? Wewe ni—wewe ni—wewe ni Myunani. Unajua, wewe si wa dhehebu Lake. Usishuke kwenda kule kwenye kundi lile.”

¹¹⁰ Sasa, hiyo ni mojawapo ya hizo pingamizi. Mnaona? Lakini kama unayo imani, utaenda, kwa vyovyote vile. Hiyo haileti tofauti yoyote, dhehebu alilomo, mradi tu Yeye yupo.

¹¹¹ Yeye alikuwa na haja. Alikuwa na binti aliyekuwa yuafa kwa kifafa. Naye ilimbidi kumwenda, maana madaktari hawangeweza kumfanyia lolote. Hawawezi kumfanyia bado. Kwa hiyo ilimbidi kwenda kwa Yesu. Alikuwa amesikia kwamba Yeye alikuwa ameyaponya magonjwa kama hayo.

¹¹² “Vema,” wakasema, “Yeye, Yeye si—Yeye si. . . Yeye kamwe hakuja na uamsho Wake kwenye madhehebu yenu.” Hilo halikumzuia. Maskini mwanamke huyo alikuwa na imani. Aling’ang’ania. Akalipita tu kundi hilo. Imani yake ilimvuta ikamtoa kwake.

¹¹³ Loo, laiti wangelifanya tu jambo hilo leo hii! Mtu fulani anasema, “Kuna mkutano usiku wa leo huko chini kwenye kanisa la Foursquare.”

¹¹⁴ “Vema, si wa dhehebu lenu. Afadhali usiende huko chini.”

¹¹⁵ Kaza mwendo tu upite. Imani yako inakupeleka mbele moja kwa moja. Mnaona? Imani haina pingamizi. Inaenda, kwa vyovyote vile. Hakuna kitu kitakachoikomesha. Kama nilivyosema, ina misuli mikubwa, migumu. Inayo sakafu; hao wengine wanaiogopa. Naam, bwana. Wataitoroka Hiyo, kama ndui. Wanaenda tu mbali kabisa. Hawana uhusiano

wowote na Hiyo, imani kubwa inapoinuka, kasema, “Ninajua ninayemwamini. Nimeshawishika.” Jambo ndilo hilo.

¹¹⁶ Huenda kulikuwa na kundi lingine lililokuja, likasema, “Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho. Hilo ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha huko chini, hao Wayahudi. Sisi ni Wayunani. Sisi ni werevu. Sisi ni kundi la watu wenye akili. Tumeupa ulimwengu sanaa, muziki, na—na dini. Na hakuna kitu kama Hicho.”

¹¹⁷ Lakini yeye aling’ang’ania. Siku za miujiza hazikuwa zimepita, kwake, kwa sababu kitu fulani tayari kilikuwa kimemwambia, *hapa* chini, kwamba hazikupita. Naye Yesu alikuwa na kile alichokuwa akitafuta, naye aliyakinia kumfikia. Bila kujali kama dhehebu lake liliudhamini, au la, yeye alikuwa anaenda, kwa vyovyote vile. Yeye alikuwa anaenda kule chini. Alikuwa aking’ang’ania, angali anang’ang’ania. Huenda siku za miujiza zilikuwa zimepita kwa ajili yao, bali hazikupita, kwake. Hivyo ndivyo ilivyo na kila mwaminio. Hao watu wanasema siku za miujiza. . .

¹¹⁸ Mtu fulani aliniambia, wakati fulani uliopita, kasema, “Sijali ungesema nini, Bw. Branham.” Kasema, “Siamini kuna kitu kama uponyaji wa Kiungu.”

¹¹⁹ Nikasema, “Bila shaka hakuna, kwako. Haukuwa ni kwa ajili ya wasioamini. Kwa hao tu wanaoamini. Hiyo ni kweli. Haukutumwa kwa wasioamini. Ulitumiwa waaminio. Huwezi kuufurahia, kwa kuwa hujui lolote kuuhusu Huo.”

¹²⁰ Yeye alitaka kuniambia, “Hakuwa na kitu kama Roho Mtakatifu.”

¹²¹ Nikasema, “Umechelewa tu kupita kiasi kwa yapata miaka thelathini na mitatu, kwa hilo.” Nikasema, “Ninajua vema zaidi. Tayari nimempokea Huyo.”

“Aa, upuuzi huo!”

¹²² Nikasema, “Huenda ikawa, kwako wewe, bali si kwangu mimi. Ni halisi kwangu. Ni Uzima, kitu kilichotia nanga.” Alikuwa amechelewa kupita kiasi kuniambia hivyo.

¹²³ Wamekuja wamechelewa kupita kiasi kutuambia kuhusu uponyaji wa Kiungu. Tayari tumeponywa. Tayari tumejazwa na Roho Mtakatifu. Tayari tunayo neema ya Unyakuo. Amina. Imechelewa sana kwa lolote la mambo hayo. Ni afadhali wanyamaze. Tayari tumeupata. Imani yetu inaweza kusema, “Keti chini. Ninajua ninalozungumzia.”

“Vema, madaktari?”

¹²⁴ Sijali yale Dk. *Nanii* anayosema. Biblia ilisema hilo, nami ninayo imani katika Kitabu hicho kilicho mkononi mwangu. Nayo imani yangu inaishikilia huko nje, “Yesu yuaja. Ninaamini ya kwamba nilimpokea Roho Mtakatifu, maana ninamwona akiishi maishani mwangu.” Amina. Ni kulingana na Neno.

Hakuna kitu. . . Ufunuo uliodhihirishwa, thibitisho kamilifu la Biblia kuwa ni kweli, na Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Acheni wacheke namna hiyo. Wanaweza wakacheke watakavyo. Tutang'ang'ania tu kama walivyokuwa wakati Nuhu alikuwa, Musa alikuwa, hao waigaji wote walipoinuka.

125 Yane na Yambre walitupa fimbo yao chini, ikawa nyoka. Kulikuwako na hao watu, waheshimiwa tu kama walivyoweza kuwa, waliofanya vile hasa Mungu alivyowaambia kufanya, ndipo likatokea kundi la waigaji, wakatupa fimbo zao chini. Jambo pekee wangeluweza kufanya, ni kusimama tu kimya na kuona utukufu wa Mungu. Amina.

126 Mungu atalitetea. Kama Yeye alikutuma, nawe una hakika nayo, utafanikisha ile kazi Mungu aliyokukusudia tangu zamani ukaifanye. Utasimama pale, naye Mungu ataondoa kila mwigaji wa kimwili kutoka kwako. Kweli. Simama pale. Unaweza kung'ang'ania, kwa sababu unamjua Yeye uliyewamini, na yaliyo sahihi. Uchunguze ufunuo wako kwa Neno. Kama ni kinyume na Neno, achana nao. Kama uko pamoja na Neno, Mungu ana wajibu, anawajibika, kulitimiza Neno Lake.

127 Sasa, sasa, huenda kulikuwako na kundi la kina mama waliosimama kule chini pembeni, mwajua. Nao wakasema, "Huyu hapa anakuja. Sasa anaye yule mtoto huko juu, aliye na kifafa. Na—naye Dk. *Nanii* alisema ya kwamba—ya kwamba hakuna tiba ya kifafa. Naye huyu hapa, akishuka kwenda kwenye lile dhehebu lisilotambulikana kule, kusudi yule nabii mshupavu aje hapa na kumponya mtoto yule." Kwa hiyo wao wakasema, "Inatupasa kumkomesha Susie." Natumaini hakuna Susie hapa. "Bali inatupasa kumkomesha Susie na kumwambia, kwa sababu yeye amekuwa mwanamke mzuri. Hakuna kitu dhidi ya maisha yake. Bali inatubidi kumzuia, na ndilo jambo la pekee nijualo kufanya. Amepita, wengine wote, basi hataktivunja kizuizi hiki.

128 "Unajua nini, Susie? Mume wako atakuacha. Kwa sababu, yeye ni mdhamini ama shemasi kwenye halmashauri, naye atakuacha, hakika kabisa, kama ukienda huko chini."

129 Alikuwa angali ameshikilia. Akasonga mbele moja kwa moja. Mnaona? Imani haijui kizuizi chochote. Haina budi kufika kule.

130 Kisha akalipita kundi lingine lililosema, "Unajua nini? Utakaporudi, umeshindwa, na kuona kwamba hakuna kitu kwake, kila mtu katika ujirani atakucheka."

131 Hilo hata halikuyafanya masikio yake kuwa mekundu. Alikuwa anang'ang'ania. Akaendelea moja kwa moja. Ninapenda hilo. Ninapenda huko kung'ang'ania.

132 Ndipo hapa akasimama mmoja wa mashemasi, na kusema, "Kama ukienda huko chini, unajua watakalofanya? Watakufukuza kanisani mwako, maana umeshirikiana na

hao watakatifu wanaojibingirisha, ama hao watu.” Ndipo akasema, “Unajua...” Samahani. Labda sikupaswa kusema hilo. Mnaona? “Unashirikiana nao. Utafukuzwa kanisani mwako.”

¹³³ Alikuwa angali ameshikilia. Imani haijui kushindwa. Alikuwa na jambo moja la kufanikisha, na hilo lilikuwa, kumfikia Yesu. Alikuwa na haja, na Yeye Ndiye pekee aliyekuwa na haja hiyo.

¹³⁴ Ninasema hili usiku wa leo, ndugu na dada. Nina umri wa miaka hamsini na mitatu. Nimekuwa nikimtumikia tangu nilipokuwa na kama ishirini. Yeye amekidhi kila kitu nilichokuwa na haja nacho. Na itakapofikia kwenye saa ya kufa kwangu, nina hakika kile ninachohitaji wakati uo huo basi, mabawa mawili nipate kuuvuka ule mto, Yeye atakuwa hapo. Msiwe na wasiwasi. Ninajua Yeye atakuwa hapo. Nitarudisha tu maskini ule upanga kwenye ala, nivue helmeti, niiweke chini kwenye ule mto, wakati mimi... ufukoni, nitakapovisikia vishindo vya mawimbi yakikatika. Nami nitapaza sauti “Tuma mashua okozi. Naja nyumbani, asubuhi ya leo.” Itakuwepo. Naam, bwana. Ile Nyota ya Asubuhi itashuka na kuiangaza njia. Tutauvuka ule mto. Naam, bwana. Amina.

¹³⁵ Yeye aling’ang’ania. Alifanikiwa. Alijua kwamba ilibidi awe mvumilivu apate kumfikia Yesu, kwa hiyo ilimbidi kupita kila kitu.

¹³⁶ Hatimaye, akawasili. Sasa, hatimaye, akafika hapa. Kila kitu ni shwari sasa, halafu hii hapa pingamizi nyingine inakuja. Mtu yule yule hasa aliyekuwa amekiri ana matumaini naye, yule Mtu aliyejaribu kumfikia, Yesu. Yeye akasema, “Mimi sijatumwa kwa jamii yenu.” Loo, jamani! Hilo si lingetufanya sisi Wapentekoste kulipuka? Humm! Humm! Jamani! “Mimi sijatumwa kwa jamii yenu.” Whiu! Huo ulikuwa mshtuko mkubwa.

Bali mnajua nini? Imani haijui mshtuko wowote.

¹³⁷ Halafu basi, tena, Yeye anageuka. Baada ya mambo haya yote aliyokuwa amepitia, na imani yake ikishikilia, hata alijua Yesu angeweza kumpa shauku yake. Basi akapitia kila kimoja cha vizuizi hivi. Ndipo alipomfikia Yeye, basi akamkatalia mbali, kabisa, “Mimi hata sijatumwa kwa jamii yenu.”

¹³⁸ Ninaweza kumwazia amesimama pale, nayo macho yake yaking’aa. Yeye—yeye alikuwa mbele Zake wakati huo. Hivyo tu ndivyo alivyopaswa kuwa. Kisha kasema, “Isitoshe, jamii yenu si kitu ila kundi la mbwa.” Loo, jamani!

¹³⁹ Vipi kama angalikwambia wewe hilo? Ungalisema, “Nitachukua makaratasi yangu kutoka kwenye hii Foursquare niende mahali pengine. Kamwe sitarudi huko tena. Nitayachukua kutoka kwa *Fulani-na-fulani*.” Loo, naam. Naam, bwana.

¹⁴⁰ Lakini hata hivyo alishikilia. Loo! Mnaona? Imani haijui kushindwa. Hakuna kitu kitakachoizua. Ingawa Yesu alimwambia, Yeye yule aliyemjia, kasema, “Sikutumwa kwa jamii yenu, nao si kitu ila kundi la mbwa.” Whiu! Lakini nini? Yeye aliishikilia imani halisi. Imani haijui kushindwa; sijali inatoka wapi. Haijui kushindwa, kwa sababu alikuwa na imani. Angali alishikilia. Loo! Ninapenda hilo. Yeye hakuwa mmea wa tuta, chotara, kama baadhi yao siku hizi.

¹⁴¹ Hizi dini chotara tulizo nazo siku hizi, mwajua. Hazifai kitu. Kila kitu sasa ni chotara, chotara. Hata wana makanisa chotara, Wakristo chotara, wanaoingizwa kwa kupeana mikono. Loo, wanaweza kuvalia vizuri zaidi, labda watumie Kiingereza bora zaidi, na kadhalika, namna hiyo. Hamna uhai ndani yake.

¹⁴² Hebu chukua punje nzuri kubwa ya mahindi, chotara, labda inaonekana nzuri maradufu kuliko hiyo nyingine. Ipande, itakufa. Haina uhai ndani yake. Hiyo ni kweli.

¹⁴³ Hatutaki chochote chotara. Tunataka kitu halisi. Kama hunacho, kaa hapo mpaka kitakapokuja. Kwa nini kukubali kibadala wakati mbingu za Kipentekoste zimejaa yaliyo halisi? Unaona? Hakuna kitu chotara, hakitasimama.

Inakubidi sikuzote kunyunyizia mmea chotara, kuukinga na wadudu.

¹⁴⁴ Hivyo ndivyo walivyo baadhi ya hawa Wakristo chotara. Inakubidi kuwabembeleza na kuwapapasapapasa, na kuwaahidi watakuwa shemasi ama kitu kingine, kuwakinga na baadhi ya wadudu wa kilimwengu, wa kutokuamini. “Wangetoka kanisani.” Wafukuze, kwa vyovyote vile. Hiyo ni kweli. Kamwe hawakuwa ndani.

¹⁴⁵ Huwezi kujiunga na Kanisa. Huenda ukajiunga na chama. Unaweza ukajiunga na chama cha Methodisti, chama cha Baptisti, ama chama cha Kipentekoste. Lakini kama kamwe ukimjia Kristo, utazaliwa katika lile Kanisa, hiyo ni kweli, Mwili wa kisiri wa Kristo. Mengine ni vyama. Hiyo ni kweli. Ni sawa, sina kitu dhidi yao. Lakini unazaliwa katika Kanisa la Mungu aliye hai, kwa Roho wa Mungu. Huwezi kujiunga na Hilo, hata kidogo. Basi wakati unapozaliwa Mle, una Kuzaliwa.

¹⁴⁶ Wewe si chotara tena, mwenye kujiunga kwa kupewa mkono ama mwomba lifti. A-ha. Unajua, mwomba lifti sikuzote anababaisha. Ndivyo hivyo. “Vema, najua, bali Dk. *Nanii* . . .” La, la. Jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo. Hiyo ni kweli kabisa.

Aling'ang'ania. Hakuwa chotara. Haikukubidi kumnyunyizia, kwa manukato, kumfanya sahihi. Alisimama pale.

¹⁴⁷ Sehemu ya mazao yetu siku hizi, mengi sana ni chotara. Ni kitu tu kama David duPlessis, ninaamini, alivyosema wakati mmoja, “Mungu hana wajukuu.”

¹⁴⁸ Shida ya mwenendo wetu wa Kipentekoste, tunawapata wajukuu wa Kipentekoste. Wanaingia kwa sababu baba na mama zetu walikuwa ni Wapentekoste. Tumewaweka kwenye orodha ya watoto, nao wanakuja bila tukio. Na hapo wanasema wao ni Pentekoste, pia. La, bwana. Mungu hana wajukuu. Yeye si babu; Yeye ni Baba. Kweli. Kama ukipata kwenda Mbinguni, utalipa gharama kama mama yako alivyofanya, baba yako alivyofanya. Amina. Hilo linaweza kusikika fidhuli, bali ni Kweli. Ni njia fidhuli ya kutoa hoja, bali mnaelewa Kiingereza cha namna hiyo, nina hakika. Si Kiingereza kizuri sana. Linaleta hoja, yale ninayotaribu kusema. Yasikilizeni tu. Naam.

¹⁴⁹ Yeye hakuwa chotara. Haikumbidi kunyunyiziwa, na kubembelezwa sasa, “Vema, sasa, dada mpendwa, na—nakwambia, vema . . .” Loo, la. La, bwana.

¹⁵⁰ Na haidhuru ni kitu gani kilichomwangusha chini, yeye alisema, “Ni kweli. Sisi si kitu ila kundi la mbwa. Ni kweli kwamba hatuustahili.” Loo, jamani! Alikubali ya kwamba Yeye alikuwa sahihi.

¹⁵¹ Nitasema jambo zito. Iweni tayari. Kila wakati, imani halisi itakubali Neno ni kweli. Na wakati wowote, ambapo kitu fulani kinasema ya kwamba siku za miujiza zimepita, ama kitu fulani dhidi ya Biblia, hiyo si imani halisi. Imani sikuzote itakubali ukweli. Huna budi kudumu na Neno. Haijalishi kitu kingine chochote kinasema nini, kile mtu mwingine yeyote asemacho, Neno ndilo kweli. “Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe kweli. Yeyote atakayeongeza kwake, au kuondoa kwake, huyo ataondolewa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima.”

¹⁵² Ati Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kanisa? Lipi? Katoliki? Madhehebu mia sita na sitini na kitu mbalimbali? Atafanyaje hilo?

¹⁵³ Mungu atauhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo. Naye Kristo, “Hapo Mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa kwetu.” Mungu na Neno ni mmoja. *Hili* ni Mungu katika maandishi.

¹⁵⁴ Unaye—unaye Roho Mtakatifu? Panda hiyo Mbegu hapo ndani. Inaipa Uzima, inauvunja Uzima huo, na kuudhihirisha na kuuthibitisha. Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 12, “Yeye aniaminiye Mimi . . .” Yohana Mtakatifu 14:12, hasa, “Kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Kwa hiyo sikuzote huikubali Kweli. Loo, jamani!

¹⁵⁵ Lakini, mnajua, yeye alisema, “Hiyo ni kweli. Sisi si kitu ila kundi la mbwa. Na sisi si . . . Wewe kweli hukutumwa kwetu. Lakini, Bwana, sitafuti mikate yote waliyokuwa nayo watoto. Ninatafuta tu makombo.” Loo, jamani!

¹⁵⁶ Sasa, mliona? Watu, wao wanataka kumfanya *huyu*, aponywe, na kumpata Roho Mtakatifu jinsi wanavyofikiria

wanapaswa kumpata. “Sasa, nitashuka nije, ndugu, kama utanipandisha na kunipeleka kwenye chumba ambamo hamna mtu atakayeniona, kisha uweke mikono yako juu yangu na kunibariki, na kumweka Roho Mtakatifu ndani yangu. Nitamkubali.” Loo, la.

¹⁵⁷ Naamani alitaka kuukubali uponyaji wake namna hiyo, wakati mmoja. Lakini Eliya akamwambia atoke aende huko nje kwenye maskini mto Yordani wenye matope akajitumbukize mara saba. Ninaweza kumwona tu akitoka kwenye gari lake la farasi. Loo, mtu mashuhuri, akishikilia pua yake. Huyu hapa anakuja, kutoka majini, akienda kwa vidole vya miguu kama paka kwenye sukari ya rojorojo, mwajua, akitoka namna *hii*, mwajua, akitoka namna *hiyo*, akaingia majini. Akasema, “Loo, ninachukia kufanya hivi,” kudidimia-didimia chini. Watu wengine huja madhabahuni kana kwamba lilikuwa ni jambo la kuchukiza kwao. Naam. “Loo, sitaki kufanya hivyo.”

Alijitumbukiza mara moja, kisha, “Na bado ningali nina ukoma.”

¹⁵⁸ “Nabii alisema, ‘Mara saba.’” Kweli. Mpaka alipolitii Neno, kabisa! Mpaka utakapolitii Hilo, kabisa! Yeye alikuwa na mtu mzuri aliyesimama ufukoni, kasema, “Nabii alisema, ‘Mara saba,’ baba. Unaona? Endelea tu kujitumbukiza.”

¹⁵⁹ Jambo ndilo hilo. Usipoupata usiku wa kwanza, jitumbukize tena kesho yake usiku. Endelea tu mpaka u—uupate.

¹⁶⁰ Sasa kumbukeni. Yeye alikuwa kama Rahabu kahaba, maskini mwanamke huyu alikuwa hivyo. Hakuwa amewahi kuona mwujiza. Alikuwa tu amesikia kuhusu mwujiza. Ni nini yeye siku kwenye... atatufanyia nini katika Siku ya Hukumu? Kamwe hakuwa ameona mwujiza. Alikuwa ni Mmataifa. Hakuwa ameona kamwe, bali alikuwa amesikia. Nasi tumeona na kusikia, na tungali tunatilia shaka. Loo, jamani!

¹⁶¹ Yeye alikuwa kama Rahabu kahaba. Wakati wale wapelelezi walipokuja huko, haikumbidi kusema, “Nitawaambia. Mleteni Yoshua huku na afanye ibada kwa ajili yangu, nami nitaona jinsi anavyozichanua nywele zake, na jinsi anavyozungumza, na adabu anayotumia mimbarani. Nami nitaona kama ninaweza kumkubali ama sivyo.” Yeye alisema, “Nimesikia kwamba Mungu wa Mbinguni alikuwa pamoja nanyi, na jambo pekee ninaloomba ni kuokolewa.” Haya basi.

¹⁶² Maskini mwanamke huyo kweli alikuwa aking’ang’ania. Alishikilia moja kwa moja. “Niokoeni tu. Nitafanya lolote mnalotaka nifanye.” Loo, haya basi. Jambo ndilo hilo.

¹⁶³ Maskini mwanamke huyu, haijalishi shida ilikuwa ni nini, aling’ang’ania. Loo! Alikuwa na mtazamo sahihi kwa karama ya Mungu. Alikuwa na mtazamo sahihi, unyenyekevu. Alimsujudu miguuni Pake, naye alikuwa na unyenyekevu. Hakusimama, aseme, “Sasa, Wewe ngoja kidogo. Unajua sisi watu ni

Wayunani. Unasema tulikuwa mbwa. Hebu kidogo hapa, Bwana. Hivi unatambua kwamba sisi—sisi ndio mabingwa wa sanaa, nasi ndio mabingwa wa *hiki-na-hiki* na *hiki-na-kile*?” Kamwe hakuwazia hilo, hata kidogo. Alikubali tu kwamba Yeye alikuwa sahihi, kisha akasujudu miguuni Pake, na kusema, “Nisaidie, Bwana. Nitakula tu makombo. Iwapo binti yangu hawezi kupata kipande kizima cha mkate, utamruhusu tu apate makombo, kama yeye ni mbwa?” Loo, jamani! Haya basi.

¹⁶⁴ Tungeridhika na makombo tu, kama Roho Mtakatifu angemfunulia mtu fulani usiku wa leo, “Umeponywa”? Hivi mngekuwa tayari kuchukua tu makombo, ama mngetaka Mungu kuja huku na kuwainua juu na kuwapa namna fulani ya hisia? Kama Yeye angesema tu moyoni mwako, “Ugonjwa wangu umekwisha. Hunao tena. Ninaamini kwamba nitaponywa, tangu usiku wa leo na kuendelea,” ungeyachukua makombo? Ama, ungetaka kila mtu aje na kukuwekea mikono, na kumimina mafuta, na kupitia utaratibu wa kawaida namna hiyo, ama unatafuta tu makombo? Mungu ataheshimu hilo.

¹⁶⁵ Mnajua, wengi wa wanafunzi walikuwa wamemwona baada ya kufufuka Kwake. Tomaso akasema, “La, salaale, sitaamini. I—itanibidi kutia mikono yangu kwenye makovu, ya misumari Yake mikononi Mwake na ubavuni Mwake. Ndipo nitaamini.”

¹⁶⁶ Akasema, “Njoo hapa, Tomaso.” Kasema, “Niguse.” Naye akamgusa.

Akasema, “Bwana wangu, na Mungu wangu.”

¹⁶⁷ Akasema, “Tomaso, kwa maana umeona na kugusa, na kila kitu, umesadiki.”

“Naam, Bwana.”

¹⁶⁸ Yeye akasema, “Thawabu yao ni kubwa zaidi jinsi gani, ambao hawajawahi kuona na hata hivyo watamwamini!”

¹⁶⁹ Tuko tayari? Hivi sisi ni Wamataifa kama mwanamke yule Mmataifa? Yeye alikuwa ni mfano kwetu sote, “Nipe tu makombo, Bwana?” Hebu nimsikie tu mtu fulani, “Kamwe sijapata kulisoma Neno, lakini niambie kwamba Wewe unawaponya wagonjwa. Makombo hayo yatanitosha. Ninaamini hilo. Hebu nimsikie mtu fulani akisema, na kulisoma kutoka kwenye Neno, ya kwamba Roho Mtakatifu. . .”

¹⁷⁰ Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, hata wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

¹⁷¹ “Bwana, ninajisikia kwamba hilo ni kweli.” Hayo ni makombo. Njoo huku. Hayo ndiyo yote yakupasayo kufanya. Njoo.

¹⁷² Tuko tayari kula makombo? Tuko tayari kujinyenyekeza? Yeye alikuwa tayari. Alikuwa tayari kujinyenyekeza. Imani sikuzote hukubali Neno ni kweli. Sikuzote imani ni nyenyekevu. Imani hujinyenyekeza. Sasa, yeye alikuwa akitafuta tu makombo.

¹⁷³ Angalia aliyosema Yesu. “Kwa neno hili, kwa neno hili, ‘Niko tayari kula makombo, Bwana.’ Kwa neno hili, mtoto wako amepona. Umepokea haja yako kwa sababu unaiamini.”

¹⁷⁴ Imani hukubali ya kwamba Neno la Mungu ni kweli. Imani huyakubali mambo haya yote.

¹⁷⁵ Martha, Mariamu; kote katika Biblia tungeweza kuwaita wengi; yule mwanamke Mshunemi. Vitu vingi na visa ambavyo tungeviita. Hatuna wakati wa kufanya hivyo. Juu ya hili, ninazo karibu kurasa tano hapa, zilizoandikwa za watu, sasa, walioyaendea makombo. Lakini hebu tuyapite hayo kwa dakika moja tu. Ninamhisi Roho Mtakatifu akiwa karibu. Sidhani ni muhimu.

¹⁷⁶ Hebu niwape tu tukio moja dogo. Wafanyabiashara waliandika kile kitu kidogo mle ndani, yale makala mafupi sio muda mrefu uliopita, katika gazeti lao. Basi kumbuka, unapochapisha kitu, heri uweze kukiunga mkono. Tunayo, taarifa iliyoandikwa kutoka kwa daktari. Nimeona, humu kanisani usiku wa leo, Wahispaniola wengi tu.

¹⁷⁷ Nilikuwa katika Jiji la Meksiko, nasi tulikuwa na mkutano adhimu sana. Nilikuwa huko yapata siku tatu usiku. Na kulikuwako na mtu niliyemwita Mañana. Alipaswa kunichukua saa kumi na mbili, naye angenichukua kama saa tatu. Nami daima, maana alikuwa ni mwenda pole sana, nikasema alikuwa ni “kesho.” Mnaona? Basi tulipofika kwenye uwanja huu mkubwa ambako nilikuwa nikihubiri, iliwabidi kunipandisha ngazi hapa juu, kisha wanishushe kwa kamba, chini jukwaani.

¹⁷⁸ Usiku uliotangulia, kulikuwako na mwanamume Mmeksiko aliyekuwa amehudhuria huo mkutano. Ndipo mzee huyo, huku mvua ikinyesha, jinsi ilivyokuwa, basi alikuja jukwaani, kipofu. Naye akashuka akaja. Nikatazama. Nilikuwa na viatu vizuri, na suti nzuri. Naye maskini mzee huyo, alikuwa miguu mitupu, suruali yake ndefu imechakaa kabisa. Nami nitawaambia mkalimani wangu alikuwa ni nani, ninyi watu mnamfahamu; Ndugu Espinosa, hapa juu Sacramento, California, ndugu Mpentekoste. Alikuwa akitafsiri. Tulikuwa na yapata, katika siku hizo mbili usiku, nafikiri karibu waongofu elfu thelathini ama arobaini kutoka Ukatoliki, kuingia Ukristo na Roho Mtakatifu.

¹⁷⁹ Basi maskini mzee huyu kipofu akakaribia jukwaani. Na kama huna hisia kwa ajili ya watu unaowaombea, hakuna haja ya kuwaombea. Inakupasa kujisikia mwenyewe umepachukua mahali pao. Basi nikawaza, “Kama baba yangu

mzee angalikuwa hai, angekuwa na umri wa mzee huyo. Huyu hapa. Hana viatu.” Pia hakuwa amevaa shati. Koti kuukuu, chakavu, limejaa mavumbi; kofia chakavu mkononi mwake, imeshonwa kwa kamba. Labda mzee huyo kamwe hakuwa amewahi kula chakula kizuri maishani mwake. Halafu basi jinsi hali ilivyokuwa haina huruma kwake, huyo hapo akiyumbayumba katika upofu. Macho yake yalikuwa meupe.

¹⁸⁰ Nilimwangalia jamaa huyo mzee, nami ni—nikamkumbatia tu. Naye Ndugu Espinosa asingeyafasiri maombi. Ni—nikasema, “Baba wa Mbinguni, kama ningaliweza kumpa viatu vyangu, ningevitoa kisiri asije mtu akaviona, nimpe koti langu, nimwache aende zake. Lakini yeye ni mkubwa zaidi kuliko nilivyo mimi. Ila, Mungu, mrehemu. Mrejeshee kuona kwake.”

¹⁸¹ Akapiga mayowe, “Gloria a Dios.” Nikatazama huku na huku. Angeweza kuona vizuri kama nilivyoweza.

¹⁸² Kesho yake usiku kulikuwako na shubaka, ama matita, marefu kama jengo hili, yapata urefu *huu*, bila kitu ila shali na nguo zilizochakaa.

¹⁸³ Uchumi wa Meksiko una urari mbaya. Pedro anapata... yeye ni mwashi wa matofali, huenda akapata peso kumi na sita kwa siku. Lakini itachukua siku nne za kazi kujinunulia jozi ya viatu. Lakini itambidi kuweka akiba ya kutosha katika hizo apate kugharamia, peso kadhaa, kwa ajili ya mshumaa wa grisi wa kuwashwa kwenye madhabahu ya dhahabu kwa ajili ya dhambi zake. Hilo ndilo linanikera.

¹⁸⁴ Kuwaona hao watu wa thamani, wanakuja kule saa tatu asubuhi. Hamna viti, kuketi chini. Waliegemeana, kama kondoo malishoni. Kunanyesha! Hao wanawake, wamesimama, nywele zao zikichirizika chini, wamelowa maji, wanangoja siku nzima kwenye jua kali ama mvua, ili tu kulisikia Neno la Mungu. Loo, watafanya nini wakati Phoenix itakaposimama kwenye Siku ya Hukumu pamoja nao, wakati, makanisa mazuri kila mahali, na hata huwezi kuwakusanya waingie?

Huyo hapa mwanamke amesimama, ama mwanamume, hasa, amefunguliwa macho.

¹⁸⁵ Usiku huo nilipoingia, ilikuwa ikinyesha sana. Ndugu Jack Moore, wengi wenu mnamfahamu, Ndugu Espinosa, wengi wa hao ndugu, walikuwa jukwaani. Naye Billy, mwanangu, kwa kawaida yeye huzisambaza kadi za maombi. Naye asingeweza kuwazungumzia hao watu Kihispaniola, kwa hiyo ilimbidi kumwacha Mañana afanye hivyo. Lakini alizunguka tu kuona kwamba Mañana hakuuza kadi ya maombi. Kwa hiyo hapo ndipo tunapaswa kuangalia, mwajua, juu ya kuuza kadi ya maombi. Kwa hiyo yeye alimwangalia tu. Nao wangetembea na kuona kwamba yeye amempa *Nanii* kadi, na namna hiyo. Kwa hiyo yeye akasema...

¹⁸⁶ Akanijia, nimeanza kuhubiri. Lundo kubwa mno la—la hizo nguo zimewekwa pale juu. Jinsi walivyopata kujua ipi ni ya nani, sijui mimi. Kwa hiyo walikuwa... Nilikuwa tu ndio kwanza nianze kuhubiri, ndipo Billy akanigusa kwenye bega. Akasema, “Baba, itakubidi kufanya jambo fulani, maskini mwanamke yule pale nje.” Kasema, “Nina karibu mabawabu mia tatu, na hata hawawezi kumzuia.” Maskini msichana mdogo Mhispaniola, yapata urefu *huu*, kitu kidogo kirembo, alikuwa na mtoto mchanga aliyekufa mikononi mwake, chini ya blanketi. Naye akasema, “Mañana alisambaza kila kadi ya maombi.” Naye akasema, “Hana kadi ya maombi. Na ule pale mstari, umekuwa ukisimama, kwa ajili yao pale, kwa muda wa saa mbili zilizopita, ukikungojea wewe, uje.” Kisha kasema, “Anataka kumleta mtoto huyo aliyekufa hapa, wala hatuwezi kumzuia.”

¹⁸⁷ Loo, vema, angepanda moja kwa moja juu ya hao mabawabu, apitie mbio chini ya miguu yao, ama chochote kile. Aling'ang'ania. Alitaka kufika huko. Alikuwa amemwona kipofu yule ameponywa, usiku uliotangulia. Aling'ang'ania.

¹⁸⁸ Nikasema, “Ndugu Moore, yeye hajui mimi ni nani. Hajui nani ndiye nani. Wewe shuka tu kule ukamwombe huyo mtoto. Hilo litatosha. Yeye...”

Akasema, “Vema, Ndugu Branham.”

¹⁸⁹ Kwa hiyo Billy akamshika mkono, kama kwamba ni mimi, kwa hiyo wakashuka kupitia jukwaani. Nikageuka. Nikasema, “Nina furaha sana kuwa hapa usiku wa leo.” Nayo mikutano si ya kigeni kwenu watu wa hapa Phoenix. Moja kwa moja mbele zangu nikaona maskini mtoto mchanga wa Kimeksiko, asiye na meno, akicheka, katika ono ameketi hapa nje. Nikasema, “Ngoja kidogo. Ngoja kidogo, Ndugu Espinosa. Nenda kwenye...”

“Kuna—kuna nini?”

¹⁹⁰ Nikasema, “Nenda kwenye maikrofoni.” Nikasema, “Mwambie aje hapa.”

¹⁹¹ Akasema, “Baba,” Billy akasema, “huwezi kumleta hapa aziruke hizo kadi zote za maombi.”

Nikasema, “Mleteni hapa. Ndio kwanza nione ono.”

¹⁹² Kwa hiyo, yeye akamwita. Nao wakarudi. Huyu hapa akaja, ameshika mfarishi mkononi mwake, namna *hii*. Naye mtoto mchanga amelala pale, amekuwa maiti tangu mapema asubuhi hiyo, alikufa kwa nimonia, jamaa mdogo sana yapata urefu *huu*. Naye huyu hapa akaja, machozi yakitiririka mashavuni mwake, maskini macho yake meusi, nywele zake zikining'inia chini, maskini msichana mwenye sura nzuri sana. Akakimbia jukwaani na kupiga magoti, akaanza kulia, “Padre!”

Nikasema, “Simama, hebu kidogo.”

¹⁹³ Nikawazia, “Bwana, vipi kama siye huyo? Vipi kama huyo hakuwa ndiye? Sijui mimi. Ndiyo kwanza nimwone maskini

mtoto mchanga wa Kimeksiko, mchanga, asiye na meno, ufizi wake mdogo. Alikuwa akinicheka, ameketi moja kwa moja *huko nje.*"

¹⁹⁴ Naye alikuwa akilia. Ndipo nikaweka mkono wangu juu ya hiyo blanketi iliyolowa maji, nako kunanyesha mvua wakati huo. Nikasema, "Baba wa Mbinguni, maskini mwanamke huyu, hapana shaka niani mwangu ila kwamba Wewe unamjibu." Nikasema, "Niliona ono, ambalo Wewe unajua ni kweli, la mtoto mchanga. Ninalikubali tu kwa imani kwamba ni mtoto huyu. Simjui mwanamke huyu wala mtoto huyu mchanga. Lakini, kitu fulani, Wewe hutenda kazi miisho yote miwili ya mstari." Nikaweka mikono yangu juu yake. Basi nilipofanya hivyo, alirusha mateke na kulia kwa nguvu alivyoweza kulia. Mama akainyakua blanketi kutoka kwake, naye huyo hapo, hai, mikononi mwake.

¹⁹⁵ Nikasema, "Ndugu Espinosa, usiliandike hilo, bali mtume mtu mzuri mwaminifu." Naye mama huyo alikuwa akiwaambia katika Kimeksiko, ya kwamba daktari alimtangaza mtoto wake amekufa, kwa nimonia, asubuhi hiyo yapata saa mbili ama tatu. Naye huyu hapa baada ya saa nne, usiku huo. Nami nikasema, "Tuma mtu ukapewe taarifa iliyoandikwa, ikaidhinishwa na daktari, ambaye alitangaza kwamba amekufa."

¹⁹⁶ Basi daktari wa Kimeksiko akaandika taarifa na kuitia sahihi, "Nilimtangaza mtoto huyu amekufa, hakuna upumuaji wala chochote kile, ofisini mwangu asubuhi ya leo saa tatu."

¹⁹⁷ Naye huyu hapa, saa nne usiku huo. Basi kesho yake asubuhi, mtoto huyo mchanga alikuwa ofisini mwa daktari akachunguzwe, "Yu mzima, tena." Kwa nini? Kwa sababu maskini mwanamke huyo alishikilia.

¹⁹⁸ Imani haijui kushindwa. Kama kuna elfu tano wamesimama mahali hapo, hakuna kitu kinachochukua mahali pake. Kanisa lake lingeweza kumfukuza, majirani wake wangeweza kucheka. Bali Mungu ambaye angeyafungua macho ya mtu, usiku uliotangulia, angeweza kumfufua mtoto wake mchanga, kwa sababu Yeye ni Mungu yule yule jana, leo, na hata milele.

¹⁹⁹ Na iwapo kundi hili la watu hapa usiku wa leo, watafutaji makombo, kama ndivyo mlivyo; Mungu yeye yule aliyekuleta hapa, ambaye angeweza kukuongoza mahali kama hapa, Mungu aliyekuoka, Mungu ambaye angeweza kukujaza na Roho Mtakatifu; Mungu yuyo huyo anaweza kuondolea mbali kila maradhi na huzuni, chochote kile, mioyoni mwenu usiku wa leo, kama unaamini hilo. Kung'ang'ania, kuvumilia, nyosha mkono ukanyakue makombo hayo madogo ya imani sasa, useme, "Bwana, asante kwa hayo. Mimi hapa naja."

Jirani atasema kesho, "Hujapona."

²⁰⁰ Useme, "Loo, lakini nimepona. Nimepona. Nilipata makombo jana usiku kwenye kanisa la Foursquare. Kitu fulani

kilitia nanga ndani yangu. Hakuna kitu kitakachonizuia, tena. Ninao.”

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

²⁰¹ Unahitaji makombo usiku wa leo? Unaweza kuchukua makombo na kung'ang'ania nayo?

²⁰² Makombo madogo ya imani yanayomjia ma—maskini mwanamke Mmataifa wa Kiyunani, asiyepata kuona mwujiza maishani mwake, kafiri mwabudu sanamu, bali alisikia ya kwamba lilitendeka kwa mtu mwingine. Kamwe hakuwa ameliona, bali aliliamini. Nayo masikitiko yote aliyokuwa nayo, hata hivyo, juu ya msingi wa kitu fulani moyoni mwake kikimwambia ya kwamba mtoto wake angeweza kuponywa, mwajua, alipofika nyumbani alimkuta binti yake amelala kitandani. Kifafa kilikuwa kimemwacha. Sio tu kwa ajili ya nafsi yake, bali kwa ajili ya binti yake asiye kuwapo.

²⁰³ Unahitaji makombo usiku wa leo? Kama unahitaji, ungeweza tu kuinua mkono wako. Na kusema, “Bwana, makombo tu ndiyo niombayo.”

²⁰⁴ Ee Baba wa Mbinguni, waangalie hao Wamataifa wanaotafuta makombo. Nyakati hazijabadilika bado, Bwana. Wamesikia. Wamesikia ya kwamba Wewe huwaponya wagonjwa. Wamesikia ya kwamba Wewe hujaza na Roho Mtakatifu. Unawapa raha waliochoka. Ee Mungu, jalia kwamba hawa hapo usiku wa leo wanaolia kama maskini mama yule wa thamani wa siku nyingi zilizopita, “Bwana, hakika hatustahili kupokea baraka kama watu Wako, Israeli, bali tunatafuta tu makombo yanayoanguka kutoka mezani pa Bwana.”

²⁰⁵ Na usiku wa leo tumeonyesha Chakula kikuu ambacho umelilisha Kanisa Lako. Na usiku wa leo hatuna makombo tu, bali tumealikwa mezani. Haitubidi hasa kula makombo, bali tuna furaha kuyapata. Lakini tumealikwa mezani, usiku wa leo. “Yesu ameandaa meza Yake ambapo watakatifu wote wa Mungu wanalishwa. Yeye anawaalika watu Wake waliochaguliwa waje wale.” Tujalie, usiku wa leo, Baba, kwamba kila mmoja aliye na haja, haja hiyo itatimizwa.

²⁰⁶ Na wakati tumeviinamisha vichwa vyetu, na mioyo yetu kwa unyenyekevu mbele za Mungu, sijui tu ni watu wangapi katika jengo hili, usiku wa leo, ambao hawajaokoka, ambao kama Yesu angekuja na ulimwengu ungekutana na mwisho wake usiku wa leo. Nawe ungeninii. . . Uko tayari kuchukua makombo madogo ya imani ambayo yamewekwa moyoni mwako, na kuja mezani usiku wa leo, ukiwasilisha makombo yako madogo ya imani mbele za Mungu, nawe ungetaka kufanya hivyo, waweza kusimama tu na kushuka uje hapa, na uache tukuombe hapa madhabahuni?

²⁰⁷ Unaweza kuja pasipo kuchelewa kwokwote? Shuka tu uje. Mungu akubariki, ndugu yangu. Mtu mwingine aweza kuja?

Bwana awe pamoja nawe, dada yangu. Njoo tu hapa. Kunaweza kuwako na mtu mwingine hapa anayetaka makombo, angeshuka tu aje kwenye meza ya Bwana? Aseme, “Bwana, sistahili kuja. Mimi—mimi... Mimi ni mbwa. Ninaninii tu... Sistahili zaidi ya yule mwanamke alivyostahili, bali ninakuja nipate tu makombo.” Waweza kuja, rafiki mwenye dhambi? Njoo. Huenda ikawa ndio wakati wako wa mwisho.

²⁰⁸ Mnaona jinsi ulimwengu unavyoendelea leo? Watu hawataki kuja tena. Ni vigumu kwako kuwashawishi. Injili, inaonekana, inaenda huko nje hudumani.

²⁰⁹ Mungu akubariki, ndugu yangu mwema. Mungu awabariki. Hilo ni zuri sana. Simameni tu papa hapa kwa muda mfupi.

²¹⁰ Mtu mwingine apachukue ma—mahali hapa kando, na aseme, “Ninasimama pamoja na mtu huyu.” Bwana akubariki, mwanangu. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Shuka uje moja kwa moja, useme, “Ninataka makombo, Bwana. Makombo ni sawa kwangu. Kitu fulani kiliugusa moyo wangu. Sasa nashuka nije.” Mungu akubariki, mwanangu. Mungu akubariki, ndugu yangu. Simama papa hapa.

²¹¹ Mtu mwingine anayesikia makombo madogo moyoni mwako, ya imani, ambayo yangekushawishi uje mezani sasa. Waweza kushuka chini na hawa vijana wanaume wanne wanaosimama hapa, wakingojea? Nilihubiri kuhusu mwanamke usiku wa leo, na ni wanaume ndio wanaokuja. Vipi kuhusu hilo, dada? Hivi hutakuja, pia, kwa ajili ya makombo? Una hiyo imani ndogo inayokwambia kwamba umekosea?

Useme, “Vema, sijui makombo ni nini, Ndugu Branham.”

²¹² Makombo ni kile moyoni mwako sasa, kinachokwambia umekosea. Unapaswa kutubu. Njoo, sivyo? Simama na uje kwa utamu, upesi, kwenye chemchemi iliyojaa Damu. Hivi huwezi kutoka uje? “Nimekosea, ndugu. Niombe.” Shuka uje. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki.

²¹³ Mtu mwingine? “Ninataka tu makombo, Bwana. Makombo haya madogo moyoni mwangu, ninakuja sasa kuyawasilisha.” Hivi utakuja?

²¹⁴ Sasa kuna yeyote hapa aliyerudi nyuma, amepotea, nawe ungetaka kuja, utakuja sasa?

²¹⁵ Wengine wasio na Roho Mtakatifu, hamjampokea Roho Mtakatifu? Loo, rafiki, kama Nuru hii imefanywa halisi sana kwako, katika siku za mwisho, hivi hutakuja usimame pia? Huenda huu ukawa ndio wakati ambapo ile shauku kubwa moyoni mwako, kitu fulani kinachokwambia, “Ninaamini Bwana atanipa ubatizo wa Roho usiku wa leo. Ninataka kuja, kusimama.” Njoni kuyazunguka madhabahu. Mtafanya hivyo? Simameni pamoja nasi kwa ajili ya maombi, ninyi mnaohisi makombo madogo, kwamba, “Ninahitaji Roho Mtakatifu.”

Kama mtu anaweza kuja kote kutoka Ohio, aruke huku chini kwa ndege. Mungu akubariki, Ndugu Grant. Mpresbiteri anaweza kuruka kutoka Ohio, huku chini, kwa ndege kusimama madhabahuni, vipi kuhusu watu wa Phoenix?

²¹⁶ Mungu akubariki, dada yangu. Simama papa hapa kwa muda kidogo. Hivi hutakuja?

Kutoka kwenye mishipa ya Imanueli,

²¹⁷ Hivi hutakuja ambapo Chemchemi imefunguliwa usiku wa leo, iliyojazwa tu na vitu vizuri vya Mungu? Sijui, wakati tuingoja kwa muda kidogo tu, hakika kuna zaidi ya hao hapa ndani, ambao wangukuwa tayari kula makombo. Bila shaka kunapaswa kuwapo. Hivi hutakuja? Fanyeni tu kama ninavyowaomba, mara moja. Lichukue tu kwa uaminifu moyoni mwako, useme, “Nashuka nje. Huu ndio wakati wangu wa kuja. Naja, kwa vyovyote vile.” Mungu awabariki, enyi dada. Hilo ni zuri sana. Tunangojea sasa, kwa subira, ili uje.

²¹⁸ Na tuinamishe vichwa vyetu sasa wakati tuingoja, tuuimbe wimbo huu wa kanisa.

Kuna Chemchemi iliyojaa Damu,
Iliyotolewa kwenye ninii ya Imanueli. . .

²¹⁹ Hivi hutakuja sasa? Hutayakuchukua makombo yako uje?

. . . chini ya gharika hiyo

Kama unataka Roho Mtakatifu, mbona usije, uingie sasa?

Hupoteza waa lao lote la hatia,
Hupoteza waa lao lote la hatia;
Nao wenye dhambi wakitumbukia chini. . .

Njoo, rafiki.

Hupoteza ninii yote. . .
Mwizi aliyekuwa akifa alifurahia kuona
(...?...papa hapa madhabahuni.
Nanyi...?...)

. . .ingawa ni mwovu kama yeye,
Asafishe dhambi zao zote. . .

Mungu akubariki, ndugu yangu. Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo.

²²⁰ Sijui kama wahudumu hapa sasa wangukuwa wasimame hapa juu pamoja nasi. Wahudumu humu jengoni, njoni msimame hapa pamoja nasi, dakika moja sasa, walimu ambao—ambao wanavutiwa na nafsi zilizopotea.

. . .nijalie, ingawa ni mwovu kama yeye,
Nioshe dhambi zangu zote.

²²¹ Sijui kama wapo wahudumu hapa, walimu wa Neno, ambao wangetaka kuja. Kumbukeni, vikomo vya Milele vinaamuliwa sasa hivi. Hawa hapa kama watu saba ama wanane, kumi

wamesimama hapa. Nanyi mnajua maana ya hilo? Nafsi moja ina thamani ya dunia elfu kumi. Haitupasi kulichukua hili kwa wepesi.

²²² Sasa, ninyi mlio wagonjwa, na mnataka mwombewe maombi ya imani, naomba msimame tu papo hapo mlipo, walio wagonjwa na wahitaji. Hilo ni jema.

²²³ Sasa, ndugu zangu wahudumu, hilo ni zuri tu, wekeni mikono yenu juu ya watu hawa.

²²⁴ Sasa, enyi watu wagonjwa, simameni karibu kidogo vya kutosha, ambapo mwaweza kuwekeana mikono ninyi kwa ninyi. Sasa, Biblia ilisema, kwenu wagonjwa, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Huna budi kuwa mwaminio, la sivyo usingekuwa umesimama. “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Mnajua hiyo ni kweli. Hayo ni Maandiko yasiyoweza kushindwa.

²²⁵ Nao hawa wenye kutubu wanaokuja madhabahuni, ndugu na dada zangu wanaokuja madhabahuni usiku wa leo, wanadamu wanaojua ya kwamba huna budi kumkabili Mungu siku moja. Biblia ilisema dhambi za watu wengine huwatangulia, wengine zinawafuata. Mnakiri zenu usiku wa leo, kusudi dhambi zenu ziwatangulie, na zikasamehewe kupitia Damu ya Bwana Yesu.

²²⁶ Nanyi hapa mnaotafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu, Mungu alifanya ahadi katika Matendo 10. Tunasoma, “Wakati Petro alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia waliolisikia.” Walikuwa na njaa sana! Sasa, una njaa. Ulileta makombo hayo madogo hapa juu. Sasa hebu tuchukue mlo mzima halisi wa baraka za Mungu. Wote ni kwa ajili yako.

²²⁷ Sasa, ninyi watu mnaoamini katika maombi, hebu tuviinamishe tu vichwa vyetu pamoja na kuomba sasa na kuamini. Sasa, sahai tu ni nani aliye karibu nawe. Jua kwamba hakuna mtu aliye karibu nawe ila Yesu Kristo. Na kila mmoja aombe jinsi uombavyo, jinsi umezoea kuomba. Na, ndugu, wekeni mikono yenu juu ya watu hawa, na hebu tuamini sasa Roho Mtakatifu atakuja na kutekeleza mambo haya tunayomba.

²²⁸ Baba yetu wa Mbinguni, hatujisikii kwamba tumesimama hapa bure. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya nafsi hizi. Tunajua ya kwamba Wewe upo hapa sasa kuwaokoa. Ninaomba ya kwamba utalijalia, Bwana. Jalia imani yao iangalie kupita hicho kivuli. Jalia hawa wanaomtafuta Roho Mtakatifu, waliowekewa mikono ya waaminio, walio wagonjwa na wanaoteseka, jalia nguvu za Mungu zifanye kazi katika jengo hili, juu chini ya marefu haya, na kupitia kwa watu hawa. Kisha umwokoe kila mwenye dhambi, mjaze kila mwaminio na Roho Mtakatifu, na umponye kila mgonjwa. Tujalie mambo haya, Bwana. Ninaamini

kwamba Wewe upo hapa, na Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ahadi Zako haziwezi kushindwa.

²²⁹ Tunaamini kwamba Wewe uliliagiza Kanisa Lako, nao wakapanda kwenda kwenye mji wa Yerusalemu. Walipanda hadi kwenye chumba cha juu, nao walikuwa huko, sikuzote, wakimsifu na kumbariki Mungu. “Na mara ikaja kutoka Mbinguni sauti ya Upepo mkali ukienda kasi, nao Huo ukaijaza nyumba yote walimokuwa wamekusanyika.” Wewe ni yeye yule, na Wewe unaweza kufanya jambo lile lile. Jalia nguvu, zilizoshuka chini kwenye siku ya Pentekoste, zibatize kundi hili la watu usiku wa leo, katika nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo. Maombi haya ninaomba katika Jina la Yesu, kwa ajili ya watu hawa, kwa utukufu wa Mungu.

²³⁰ Inueni mikono yenu sasa. Maombi ya imani yameombwa, maombi ya imani ya msamaha. Inueni mikono yenu msemi, “Bwana asifiwe.” Anzeni tu kumsifu Yeye na kumbariki. Kiri tu dhambi zako. Ki- . . . Amini kwa moyo wako wote. Inueni mikono yenu kwa Mungu, msemi, “Asante, Bwana Yesu. Ninaamini, dakika hii, Wewe utanipa Roho wa Bwana, ulinibatiza kwa Roho Mtakatifu na kunipa baraka.”

Vema, dada, njoo . . . ? . . .



KUNG'ANG'ANIA SWA63-0113E

(Perseverance)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili jioni, tarehe 13 Januari, 1963, kwenye Kanisa la Foursquare huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org